



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2012



Jani la Bangi




Mirungu



Heroin



Cocaine



Amfetamini



Imetayarishwa kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria ya
Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya [Sura ya 95]



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2012



Imetayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia
Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya [Sura ya 95].

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2012 imeandalowi na:

Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya,
S.L.P. 80327,

Kitalu Namba 434, Barabara ya Malik,
Upanga, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2152532
Tarakilishi: +255 22 2152820
Barua pepe: tumedawa@pmo.go.tz
Tovuti: www.pmo.go.tz

ISBN: 978-9987-9596-4-8

MAELEZO YA WAZIRI

Nchi yetu bado inakabiliwa na tatizo la matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya. Tatizo hili limechangiwa na mambo mbalimbali yakiwemo uelewa mdogo juu ya tatizo lenyewe, mmomonyoko wa maadili na uchu wa kujipatia utajiri wa haraka. Matumizi na biashara ya dawa hizi yamesababisha, madhara makubwa katika jamii yetu yakiwemo kuongezeka kwa magonjwa ya afya ya akili, kudhoofika kwa afya za watumiaji, kuenea kwa magonjwa ya ambukizi kama vile homa ya ini, kifua kikuu na VVU/UKIMWI hasa kwa wajidunga. Vilevile, matumizi ya dawa hizi huathiri uwezo wa watumiaji kufanya kazi na kusababisha kupungua kwa ufanisi na hatimaye kudidimiza uchumi. Vitendo vinavyoambatana na matumizi na biasharya dawa za kulevya vikiwemo wizi, ubakaji, ajali za barabarani na utupaji ovyo wa sindano za kujidunga vimekuwa vikihatarisha amani, usalama na afya kwenye jamii.

Serikali imechukua hatua mbalimbali kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya nchini. Katika kipindi cha mwaka 2012, jitihada zilizofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zilikuwa ni pamoja na kukamata na kuharibu dawa za kulevya zilizoingizwa au kusafirishwa kwenda nchi za nje, kuwakamata watuhumiwa waliojihuisha na biashara hiyo na kuwachukulia hatua za kisheria. Mwaka 2012 uliongoza kwa kukamata kiasi kikubwa cha dawa za kulevya kwa wakati mmoja ambapo kilo 211 za heroin zilikamatwa mkoani Lindi. Aidha, ekari 214 za mashamba ya bangi ziliteketezwa. Sambamba na kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya, huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevya zilipewa kipaumbele ambapo kituo cha tiba kwa watumiaji wa heroin kilifunguliwa katika Hospitali ya Mwananyamala jijini Dar es Salaam. Aidha, elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ilitolewa kwa umma kwa madhumuni ya kuitahadharisha jamii juu ya tatizo lenyewe, kukuza mitizamo inayochukia dawa za kulevya na kufafanua mikakati inayotekerezwa na Serikali kuondokana na tatizo hilo.

Mwaka 2012, Serikali ilianzisha mchakato wa kuanda Sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya ili kuwa na mwongozo thabiti wa kitaifa wa kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya kikamilifu. Sera hii itakapokamilika itahitaji ushiriki wa wadau wote kutokomeza kwa pamoja tatizo la dawa za kulevya nchini. Aidha, katika kuimarisha udhibiti wa uingizaji na usafirishaji haramu wa dawa za kulevya nchini, Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya [Sura 95] ilifanyiwa marekebisho ambayo pamoja na mambo mengine sheria hiyo imeongeza adhabu kwa watu watakaopatikana na hatia ya kujihuisha na biashara haramu ya dawa za kulevya, lengo likiwa kuwaogopesha watu wanaofanya biashara hiyo na wale wenye nia ya kutaka kujiingiza kwenye biashara hii wasifanye hivyo.

Udhibiti wa dawa za kulevyta unahitaji mfumo thabiti wa kitaasisi unaoshirikisha vyombo vinavyopambana na biashara haramu ya dawa za kulevyta pamoja na taasisi zinazojihusisha na udhibiti wa matumizi ya dawa hizo. Kwa kuzingitia hili, Serikali iliendelea na mchakato wa kupata chombo kipyta chenye nguvu kitakachoimarishe mapambano dhidi ya dawa za kulevyta.

Dawa za kulevyta hutishia mustakhbali wa taifa na huathiri afya na ustawi wa jamii ya watanzania na dunia kwa ujumla. Tatizo hili linahitaji ushirikiano wa dhati kutoka kwa wadau wa ndani na nje katika kupambana nalo ili kulinda haki za binadamu na afya zao, kulinda usalama wa nchi na kujenga uchumi endelevu. Hivyo, napenda kuwahimiza wananchi wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali katika kupambana na tatizo hili. Sote kwa pamoja tujenge jamii yenyeye afya bila dawa za kulevyta.



William V. Lukuvi (MB)
**Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu
(Sera, Uratibu na Bunge)**

DIBAJI

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevy ya Mwaka 2012 imeandaliwa ili kuwapa fursa wananchi kujua hali ya tatizo la dawa za kulevy na jitihada zilizofanywa na Serikali pamoja na taasisi mbalimbali katika kukabiliana na tatizo hili. Taarifa hii imejumuisha hali ilivyo katika usafirishaji wa dawa za kulevy na matumizi. Changamoto na mipango ya baadae ya kukabiliana na tatizo hili imeainishwa.

Taarifa imegawanyika katika Sura tano. Sura ya Kwanza inaonesha mwelekeo wa tatizo la dawa za kulevy nchini kwa mwaka 2012 ambapo, matumizi na mwelekeo wa dawa za kulevy ambazo ni bangi, mirungi, heroin na cocaine vimeainishwa. Aidha, Sura hii inaelezea baadhi ya vichocheo na sababu za watu kujiingiza katika matumizi ya dawa hizi ambavyo ni shinikizo rika, ukosefu wa ajira, ukosefu wa malezi bora na uelewa mdogo juu ya madhara ya dawa za kulevy. Pia, baadhi ya maeneo yaliyoathirika zaidi kwa kilimo cha bangi na matumizi ya dawa hizo yameanishwa.


Sura ya Pili inaelezea mwelekeo wa tatizo la dawa za kulevy duniani ambapo uzalishaji, usafirishaji na matumizi ya aina mbalimbali ya dawa hizo kwa Bara la Afrika, Amerika ya Kati na Caribbean, Amerika ya Kaskazini, Amerika ya Kusini, Ulaya, Asia na Ocenia vimeainishwa.

Sura ya Tatu inaeleza udhibiti wa tatizo la dawa za kulevy nchini. Sura hii imegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni udhibiti wa upatikanaji wa dawa za kulevy, udhibiti wa matumizi wa dawa hizi pamoja na masuala mtambuka. Udhibiti wa upatikanaji wa dawa za kulevy unajumuisha uchunguzi uliofanikisha ukamataji wa dawa za kulevy, udhibiti wa kilimo cha bangi na mirungi, udhibiti wa dawa za tiba zenyе madhara ya kulevy pamoja na udhibiti wa kemikali bashirifu. Kazi zilizofanyika katika Utoaji wa elimu kwa umma na huduma za tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevy imeelezwa kwenye sehemu ya pili ya sura hilo. Sehemu ya tatu ya sura hii inaelezea masuala mtambuka ambapo kazi zilizofanyika ni mwendelezo wa mchakato wa uboreshaji wa mfumo wa udhibiti wa dawa za kulevy nchini, uwezeshaji wa asasi za kiraia na ufuutiliaji na tathmini ya udhibiti wa dawa za kulevy nchini kwa mwaka 2012.

Sura ya Nne inaainisha kazi zilizofanyika katika kudhibiti maambukizi ya Virusi vya UKIMWI mionganoni mwa watumiaji wa dawa za kulevy. Sura ya tano inaelezea mafanikio ya udhibiti wa dawa hizo yaliyopatikana kwa mwaka 2012, matatizo pamoja na changamoto zilizojitokeza wakati wa udhibiti. Mikakati ya baadae katika kuendeleza udhibiti pamoja na mapendekezo yenye lengo la kufanikisha

mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya kwa miaka ijayo ili kujenga jamii
huru isiyo na dawa za kulevya yametolewa kwenye sura hii.

Taarifa ya Hali ya dawa za Kulevya ya mwaka 2012 imeandalika kwa kuzingatia
michango ya taarifa za udhibiti wa matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya
zilizowasilishwa na wadau. Vilevile, taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani
iliyotolewa Mwaka 2013 na Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya iliyandalika
na Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya zimetumika katika kuanda
taarifa hii. Ninawashukuru wadau wote waliowasilisha taarifa zao kwa wakati na
ninawaomba wajitahidi kuwasilisha taarifa zao kila wanapotakiwa kufanya hivyo ili
kufanikisha maandalizi ya Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya kwa siku zijazo.



Aida Tesha

Kaimu Kamishna

Tume ya Kuratibu Udhhibit wa Dawa za Kulevya

YALIYOMO

MAELEZO YA WAZIRI.....	iii
DIBAJI	v
YALIYOMO	vii
VIFUPISHO	ix
SURA YA KWANZA:	1
1 MWELEKEO WA TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA NCHINI.....	1
1.1 Biashara ya Dawa za Kulevya Nchini	1
1.1.1 Bangi	1
1.1.2 Bangi iliyosindikwa.....	3
1.1.3 Mirungi	5
1.1.4 Heroin.....	7
1.1.5 Cocaine	9
1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Nchini	11
SURA YA PILI:.....	13
2 MWELEKEO WA TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI	13
2.1 Afrika	13
2.1.1 Uzalishaji na Usafirishaji.....	13
2.1.2 Matumizi na tiba	16
2.2 Amerika.....	17
2.2.1 Amerika ya Kati na Caribbean	17
2.2.2 Amerika Kaskazini.....	19
2.2.3 Amerika ya Kusini	21
2.3 Ulaya.....	23
2.3.1 Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji.....	23
2.3.2 Matumizi.....	24
2.4 Asia	25
2.4.1 Mashariki na Kusini Mashariki	25
2.4.2 Asia Kusini	27
2.4.3 Asia Magharibi	29
2.5 Oceania	30
2.5.1 Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji.....	30
2.5.2 Matumizi na Tiba	31

SURA YA TATU:	32
3 UDHIBITI WA TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA NCHINI.....	32
3.1 Udhibiti wa Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya.....	32
3.1.1 Udhibiti wa Kilimo cha Mimea ya Bangi na Mirungi	32
3.1.2 Ukamataji wa Dawa za Kulevya	32
3.1.3 Uendeshaji wa Kesi na Uteketezaji wa Dawa Za Kulevya	33
3.1.4 Udhibiti wa Dawa za Tiba zenyne Madhara ya Kulevya	33
3.1.5 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu	34
3.2 Udhibiti wa Matumizi ya Dawa za Kulevya	35
3.2.1 Elimu kwa Umma	35
3.2.2 Matibabu ya Utegemezi na Urekebishaji Tabia.....	37
3.2.2.1 Huduma kwenye Vituo vya Afya vya Manispaa na Majiji	38
3.3 Masuala Mtambuka.....	40
3.3.1 Uboreshaji wa Mfumo wa Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nchini.....	40
3.3.2 Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya [Sura 95]......	40
3.3.3 Ushirikiano na Asasi za Kiraia.....	40
SURA YA NNE	41
4 UDHIBITI WA MAAMBUKIZI YA VVU MIONGONI MWA WATUMIAJI.....	41
4.1 Mazingira Wezeshi ya Utoaji Huduma.....	41
4.2 Uboreshaji wa Mbinu za Kuwafikia Watumiaji	41
4.3 Ufuutiliaji na Tathmini	41
SURA YA TANO:	43
5 MAFANIKIO, MATATIZO, CHANGAMOTO, MIKAKATI YA BAADAYE NA MAPENDEKEZO	43
5.1 Mafanikio	43
5.2 Changamoto na Matatizo	44
5.3 Mikakati ya Baadae.....	44
5.4 Mapendekezo	44

VIFUPISHO

ATS:	Amphetamine Type Stimulants
CHRP:	Centre for Human Rights Promotion
DCMC:	Dodoma Christian Medical Center
INCB:	International Narcotic Control Board
LSD:	Lysergic Acid Diethylamide
MDMA:	Methylenedioxymethamphetamine
MDM:	Medecins du Monde
MNH:	Muhimbili National Hospital
NIMR:	National Institute for Medical Research
PCP:	Phencyclidine
PEDDEREF:	People with Drug Dependence Relief Foundation
TAPP:	Tanzania AIDS Prevention Programme
TAYOA:	Tanzania Youth Alliance
TAYOHAG:	Tandika Youth Handicraft Group
TBC:	Tanzania Broadcasting Corporation
THC:	Tetrahydrcannabinol
UKIMWI:	Upungufu wa Kinga Mwilini
UNODC:	United Nations Office on Drugs and Crime
VVU:	Virusi vya UKIMWI
YCRC:	Youth Counselling and Rehabilitation Centre
YOVARIBE:	Youth Volunteers Against Risk Behaviours

SURA YA KWANZA:

1. MWELEKEO WA TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

1.1 Biashara ya Dawa za Kulevya Nchini

Biashara ya dawa za kulevya kwa mwaka 2012 iliendelea kuwepo kama inavyodhihirishwa na ukamataji wa dawa za kulevya za viwandani zikiwemo heroin na cocaine. Aidha, dawa aina ya mandrax na morphine hazikukamatwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita. Halikadhalika, bangi imeendelea kuzalishwa kwa wingi katika mikoa mbalimbali ikiwemo Tanga, Morogoro, Arusha na Mara. Vilevile, kulikuwa na matukio ya ukamataji wa mirungi ambayo iliingizwa nchini kutokea nchi jirani ya Kenya.

Sababu za kushamiri kwa biashara hii ni pamoja na urefu wa mipaka na fukwe za bahari na maziwa vyenye vipenyo vingi visivyo rasmi, upungufu wa shughuli mbadala zenye kuleta kipato cha kutosha, upungufu wa maadili kwa baadhi ya watendaji, uelewa mdogo wa madhara ya biashara hiyo mionganoni mwa wananchi na tamaa ya baadhi ya watu ya kupata utajiri wa haraka. Kijiografia, Tanzania iko katika njia kuu ya usafirishaji wa dawa za kulevya zinazotoka bara la Asia na kusafirishwa kwenda sehemu mbalimbali duniani. Aidha, kubadilika badilika kwa mbinu za usafirishaji wa dawa hizi huongeza ugumu wa udhibiti mionganoni mwa vyombo vya dola.

Heroin inayoingizwa nchini hutokea nchi za Bara la Asia hasa nchi za Iran na Pakistani na cocaine hutokea katika nchi za Bara la Amerika ya Kusini zikiwemo Colombia, Peru na Bolivia. Takwimu zinaonyesha kuwa viwango vikubwa vilivyokamatwa kwa mwaka 2012 vilisadikiwa kuititia Bahari ya Hindi. Kwa mfano, Mwezi Januari, 2012 zilikamatwa kilo 211 za heroin kwa mara moja mkoani Lindi kiasi ambacho hakijawahi kukamatwa hapa nchini. Kiasi hiki ni kikubwa ukilinganisha na kilo 179 za heroin zilizokamatwa kwa mkupuo mwaka 2011.

1.1.1 Bangi


Kiasi cha bangi kilichoteketezwa mwaka 2012 ni ekari 214 ikilinganishwa na ekari 23 zilizoteketezwa mwaka 2011. Ukamataji wa bangi kavu uliongezeka kwa asilimia 182 kutoka tani 17.3 mwaka 2011 hadi tani 48.7 mwaka 2012. Hata hivyo, ukamataji wa bangi kavu umeendelea kupungua tangu mwaka 2008 ambapo kiasi cha bangi kavu kilichokamatwa kuanzia mwaka 2002 hadi 2007 kilikuwa ni tani 2,244.6 ukilinganisha na tani 153.4 zilizokamatwa kuanzia mwaka 2008 hadi 2012. Mojawapo ya sababu kubwa ya kupungua kwa ukamataji huo ni upungufu wa rasilimali za kuendesha operesheni za ukamataji wa dawa hiyo.

Kiasi kilichokamatwa, idadi ya kesi zilizofunguliwa mahakamani na idadi ya watuhumiwa vimeonyeshwa katika jedwali Na.1,


Jedwali Na. 1: Kiasi, idadi ya kesi na watuhumiwa wa biashara ya bangi kavu mwaka 2002-2012.

Mwaka	Kiasi (Tani)	Idadi ya Kesi	Idadi ya Watuhumiwa
2002	111.5	3674	4,711
2003	733.2	2310	1,816
2004	964.1	2120	3,634
2005	150.5	2790	3,949
2006	225.3	4880	6,215
2007	60.0	5466	7,161
2008	76.4	4463	5,670
2009	56.2	7130	3,382
2010	4.03	-	11
2011	17.3	-	39
2012	48.7	-	5548


Kielelezo Na.1: Kiasi cha bangi kavu kilichokamatwa mwaka 2002-2012



Kielelezo Na.2: Idadi ya kesi za watuhumiwa wa bangi kavu mwaka 2002-2012.



Kielelezo Na.3: Idadi ya watuhumiwa waliojihuisha na bangi kavu mwaka 2002-2012




1.1.2 Bangi iliyosindikwa

Ukamataji wa bangi iliyosindikwa uliendelea kupungua tangu mwaka 2008, ambapo kwa mwaka huo jumla ya kilo 10.462 zilikamatwa. Tangu mwaka 2009 hadi 2012 hakukuwa na kiasi chochote cha dawa hii kilichokamatwa. Hali hii inaonesha uwerekano wa kupungua kwa biashara na matumizi ya bangi iliyosindikwa hapa nchini. Aidha, kuimarika kwa juhudhi za udhibiti kulikofanywa na vyombo vya dola hapa nchini kumechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza upatikanaji wa dawa hii.


Jedwali Na. 2: Kiasi, idadi ya kesi na watuhumiwa wa bangi iliyosindikwa kwa mwaka 2002-2012.

MWAKA	KIASI (Kg)	IDADI YA KESI	WATUHUMIWA
2002	1,865.6	3	5
2003	0	0	0
2004	0	0	0
2005	78.75	1	3
2006	0	0	0
2007	15.03	7	154
2008	10.462	10	9
2009	0	0	0
2010	0	0	0
2011	0	0	0
2012	0	0	0


Kielelezo Na.4:Kiasi cha bangi iliyosindikwa kilichokamatwa nchini, mwaka 2002-2012.



Kielelezo Na.5: Idadi ya kesi za watuhumiwa wa bangi iliyosindikwa mwaka 2002-2012.



Kielelezo Na.6: Idadi ya watuhumiwa waliokamatwa na bangi iliyosindikwa mwaka 2002-2012.




1.1.3 Mirungi

Kiasi cha mirungi kilichokamatwa mwaka 2012 kilikuwa ni kilo 6,216 ukilinganisha na kiasi cha kilo 126 kilichokamatwa mwaka 2011. Mikoa ya Arusha, Mara na Tanga hutumiwa zaidi kuingiza mirungi kutokea nchi jirani ya Kenya ambako mmea huu ni zao la biashara. Hali hii ni changamoto kubwa katika udhibiti wa tatizo la mirungi nchini.


Jedwali Na. 3: Kiasi, idadi ya kesi na watuhumiwa wa biashara ya mirungi mwaka 2002-2012.

MWAKA	KIASI (kg)	IDADI YA KESI	WATUHUMIWA
2002	2,971.2	233	401
2003	12,002.5	254	410
2004	9,651.0	120	265
2005	1,122	233	289
2006	5,144.5	275	574
2007	2,164.6	471	648
2008	5,332.1	412	468
2009	22,904	857	365
2010	3,692.4	-	26
2011	102	-	100
2012	6,216	-	847


Kielelezo Na.7: Kiasi cha mirungi iliyokamatwa mwaka 2002-2012.



Kielelezo Na. 8: Idadi ya mesi za watuhumiwa waliokamatwa na mirungi mwaka 2002-2012.



Kielelezo Na. 9: Watuhumiwa waliokamatwa na mirungi Mwaka 2002-2012.




1.1.4 Heroin

Mwaka 2012 ukamataji wa dawa aina ya heroin ulikuwa ni kilo 260 ukiwa ni pungufu ya kilo tatu ya ukamataji uliofanyika mwaka 2011 ambapo kilo 263 zilikamatwa. Mwaka 2012 kulikuwa na ukamataji wa kiasi kikubwa cha heroin kwa mkupuo tofauti na miaka ya nyuma. Mwezi Februari, 2012 kiasi cha kilo 211 za dawa hii zilikamatwa mkoani Lindi zikiwahusisha watuhumiwa wanne. Inasadikika kuwa dawa hizi ziliingizwa nchini kupitia Bahari ya Hindi hali inayoonesha kutumika kwa Bahari hii kama njia kuu ya kusafirisha viwango vikubwa vyatya dawa za kulevya.

Jedwali Na. 4: Kiasi, kesi na watuhumiwa wa biashara ya heroin mwaka 2002-2012.

Mwaka	Kiasi (Kg)	Idadi ya Kesi	Watuhumiwa
2002	1.5	193	294
2003	4.1	131	155
2004	14.4	242	342
2005	9.9	230	269
2006	91.7	217	207
2007	16.2	168	254
2008	3.7	173	203
2009	9.0	317	122
2010	185.8	-	15
2011	264.26	303	20
2012	260	15	400


Kielelezo Na.10: Kiasi cha heroin kilichokamatwa mwaka 2002-2012



Kielelezo Na. 11: Idadi ya kesi za watuhumiwa waliokamatwa na heroin mwaka 2002-2012.



Kielelezo Na.12: Idadi ya watuhumiwa waliokamatwa na heroin mwaka 2002-2012.




1.1.5 Cocaine

Ukamataji wa cocaine hapa nchini uliongezeka mwaka 2012 ambapo jumla ya kilo 151 zilikamatwa ikilinganishwa na kilo 126 zilizokamatwa mwaka 2011. Vilevile, kiasi kilichokamatwa kuanzia mwaka 2009 hadi 2012 kilikuwa ni kilo 344.7 ambacho ni ongezeko mara 22 ukilinganisha na kile kilichokamatwa kati ya mwaka 2005 hadi 2008 ambacho kilikuwa kilo 14.7.


Jedwali Na. 5: Kiasi, idadi ya kesi na watuhumiwa wa biashara ya cocaine mwaka 2002-2012.

MWAKA	KIASI (Kg)	IDADI YA KESI	WATUHUMIWA
2002	2.461	67	180
2003	1.727	13	19
2004	0.6204	3	3
2005	0.362	19	20
2006	4.13	101	136
2007	6.638	81	138
2008	3.496	207	251
2009	4.389	336	108
2010	65	-	512
2011	128	284	30
2012	151	11	138


Kielelezo Na.13: Kiasi cha cocaine kilichokamatwa mwaka 2002-2012.



Kielelezo Na. 14: Idadi ya kesi za watuhumiwa wa cocaine mwaka 2002-2012



Kielelezo Na.15: Idadi ya watuhumiwa waliokamatwa na cocaine mwaka 2002-2012.



1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Nchini

Tatizo la matumizi ya dawa za kulevya hapa nchini liliendelea kuwepo ambapo bangi ilitumiwa kwa wingi ikifuatiwa na heroin, mirungi na cocaine. Aidha, dawa za tiba zenye madhara ya kulevya kama vile diazepam (vallium), zimeendelea kutumika. Matumizi ya dawa za kulevya hutofautiana kulingana na urahisi wa upatikanaji wa dawa hizo katika eneo husika. Kwa mfano, mikoa ya Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Singida na Dodoma , dawa inayotumika zaidi ni bangi na mirungi, wakati bangi

na heroin hutumika zaidi katika maeneo ya Dar es Salaam na Zanzibar. Dawa hizi hutumiwa kwa njia mbalimbali zikiwemo kumeza, kunusa, kuvuta na kujidunga.

Aidha, maeneo yaliyoathirika zaidi kwa utumiaji wa dawa za kulevyta ni pamoja na mikoa ya Dar es Salaam, Tanga , Pwani, Arusha, Mwanza, Mbeya, Morogoro pamoja na Zanzibar. Kundi linaloongoza kwa matumizi ni vijana ambao wamekuwa wakitumia dawa hizo katika maeneo mbalimbali kama vile viwanja nya michezo, maeneo yaliyojificha, fukwe, majengo yasiyotumika na vituo nya mabasi.

Watumiaji wengi wa dawa za kulevyta hujikuta wamejiingiza kwenye janga hilo ambalo ni gumu kujinasua kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo ni pamoja na kuiga kutokana na msukumo rika na utandawazi, migogoro ya kifamilia, ukosefu wa malezi bora, ukosefu wa stadi za maisha, msongo wa mawazo, ugumu wa maisha na umasikini. Sababu nyingine ni imani potofu kwamba matumizi ya dawa za kulevyta huongeza ufanisi na ujasiri katika kazi mbalimbali zikiwemo; muziki, masomo, uchimbaji madini, uvuvi, ujenzi, ukahaba, kilimo na ubebaji na usafirishaji mizigo. Imani hii potofu imechangia baadhi yao kushindwa kufikia malengo na kubobeza zaidi kwenye matumizi ya dawa hizo.

SURA YA PILI:

2 MWELEKEO WA TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI

Sura hii inazungumzia mwelekeo wa tatizo la dawa za kulevya katika maeneo mbalimbali duniani ikiwemo Afrika, Amerika ya Kati na Caribbean, Amerika ya Kaskazini, Amerika ya Kusini, Ulaya, Asia na Oceania. Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya Mwaka 2013¹, inaonyesha kuwa mwaka 2010 watu kati ya milioni 167 na 315 wenyе umri wa miaka 15 hadi 64 walikisiwa kutumia dawa moja au zaidi katika kipindi cha mwaka uliotangulia kote duniani, ambapo bangi ilitumiwa kwa wingi ikikadiriwa kuwa na watumiaji zaidi ya milioni 180.6.

2.1 Afrika

2.1.1 Uzalishaji na Usafirishaji

Mabadiliko ya kisiasa na kijamii yaliyotokea Afrika Kaskazini katika nchi za Misri, Libya na Tunisia kuanzia mwaka 2011 yalisababisha kulegalega kwa udhibiti wa biashara ya dawa za kulevya katika nchi hizo. Katika miaka ya hivi karibuni Afrika ya Magharibi imeibuka kuwa mojawapo ya njia kuu za kusafirisha na kupitishia dawa za kulevya hasa cocaine inayozalishwa Amerika ya Kusini na kusafirishwa hadi Ulaya ambako kuna soko kuu la dawa hizi. Inakadiriwa kuwa, katika kipindi cha mwaka 2011 kiasi cha tani 30 za cocaine zilisafirishwa kupitia katika eneo hili. Aidha, usafirishaji wa heroin na metamfetamini uliongezeka katika eneo la Afrika magharibi. Bangi imeendelea kulimwa, kusafirishwa na kutumiwa kwa wingi barani Afrika.

Heroin kutoka Afghanistan husafirishwa kupitia Pakistan, Mashariki ya Kati na kuingizwa katika nchi za Afrika Mashariki na Afrika Magharibi. Afrika Mashariki imeendelea kutumiwa kupitishia dawa za kulevya, hasa heroin. Kuongezeka kwa ukamataji wa heroin katika eneo hili kunadhihirisha kwamba dawa hii inaendelea kupitishwa na matokeo yake kiasi cha heroin hubaki na kutumiwa hasa katika nchi za Kenya, Tanzania, Mauritius na Shelia, jambo linaloongeza maambukizi ya Virusi vya Ukimwi hasa kwa wajidunga.

Miaka michache iliyopita utengenezaji, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya aina ya metamfetamini na *methcathinine* ulikuwa ukifanyika katika nchi za Kusini mwa Afrika pekee. Hata hivyo, katika kipindi cha hivi karibuni utengenezaji wa dawa hizo umeenea katika nchi za Afrika Magharibi hasa Nigeria na Ghana. Aidha, kumeendelea kuwepo majaribio ya kuchepushwa kwa kemikali bashirifu za kutengeneza dawa za kulevya aina ya amfetamini katika maeneo mbalimbali barani

¹ UNODC, (2013). World Drug Report

Afrika. Taarifa za wizi na kupotea kwa dawa za kulevyta za *ephedrine* na *pseudophedrine* katika nchi za Afrika Mashariki ni kielelezo dhahiri cha uwezekano wa kemikali hizo kutumiwa kama dawa za kulevyta na pia kutumika kutengezea aina nyingine za dawa za kulevyta katika maeneo mbalimbali barani Afrika. Mwaka 2012, kumekuwepo na usafirishwaji wa dawa mpya aina ya *tramadol* ambazo hazidhibitiwi kimataifa. Kiasi cha tani 132 za *tramadol* zilikamatwa Afrika Magharibi katika nchi za Ghana, Benin, Senegal na Togo zikitokea India.

Bangi

Uzalishaji na usafirishaji wa dawa za kulevyta aina ya bangi umeendelea kufanyika karibu katika maeneo yote ya nchi za Afrika. Nchi zinazoongoza kwa uzalishaji wa dawa hii Afrika Magharibi na Kati ni Ghana, Nigeria, Senegal, Togo na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo. Katika nchi za Afrika Kaskazini ni Misri na Morocco wakati Afrika Mashariki ni Ethiopia, Kenya na Tanzania na Kusini mwa Afrika ni nchi za Malawi, Afrika Kusini, Swaziland na Zambia.

Bangi iliyosindikwa

Bangi iliyosindikwa imeendelea kuzalishwa katika nchi za Afrika Kaskazini hasa kwenye nchi ya Morocco. Dawa hii imeendelea kuzalishwa na kusafirishwa kwenda Ulaya ambako kuna soko kubwa. Kulingana na takwimu zilizopo, bangi iliyosindikwa ambayo ilikamatwa duniani kote mwaka 2011 karibu asilimia 72 ilitokea nchini Morocco. Usafirishaji wa dawa hiyo ulifanyika kwa kutumia meli na boti ziendazo kasi kutoka bandari ya Tangier iliyopo Morocco kupitia maeneo ya Ceuta na Mellila nchini Hispania hadi nchi nyingine za Ulaya.

Nchi nyingine za Afrika Kaskazini zilizotoa taarifa ya kukamata kiasi kikubwa cha bangi ya kusindika ni Algeria ambayo ilikamatata zaidi ya tani 53 katika kipindi cha mwaka 2011. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2012 nchi hiyo ilikamatata tani 26 ya dawa hizo. Vile vile, Misri ilikamatata kiasi cha tani 18 za bangi ya kusindika.

Cocaine

Kiasi kikubwa cha cocaine kimekuwa kikisafirishwa kutoka Amerika ya Kusini kwenda nchi mbalimbali duniani. Cocaine huingizwa Afrika Magharibi kupitia Angola na Namibia na kupelekwa Afrika Kusini ambako kuna soko kubwa la dawa hizi. Katika kipindi cha mwezi Julai 2012, mamlaka za udhibiti nchini Argentina zilikamatata kiasi cha zaidi ya nusu tani ya cocaine iliyokuwa ikisafirishwa kwenda Nigeria. Aidha, cocaine imekuwa ikikamatwa katika nchi za Ethiopia, Tanzania, Msumbiji, Kenya na Uganda. Kwa mfano, mwaka 2011, Tanzania ilikamatata kilo

86 za cocaine zilizokuwa zikitokea nchini Brazil wakati Msumbji ilikamata kilo 65 zilizokuwa zikisafirishwa kupelekwa India.

Afyuni (Kasumba)

Afyuni au kasumba ni utomvu wa mmea unaojulikana kama mbaruti-afyuni au kwa kiingereza Opium Poppy. Afyuni hutumika kama dawa ya kulevyta na malighafi ya kuzalisha heroin (shumuya). Mimea inayozalisha afyuni iliendelea kulimwa katika Rasi ya Sinai nchini Misri, ingawa ni kwa kiwango kidogo. Afyuni inayozalishwa kwenye eneo hili ni kwa ajili ya matumizi ya ndani na hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa inatumika kutengeneza heroin. Dawa hii inashika nafasi ya nne mionganoni mwa dawa za kulevyta zinazotumiwa nchini Misri. Katika kipindi cha mwaka 2011 kiasi cha kilo 11 za afyuni zilikamatiwa nchini Misri.

Heroin (Shumuya)

Heroin husafirishwa kutoka Kusini Mashariki na Kusini Magharibi mwa Asia hadi Afrika na baadaye hupelekwa barani Ulaya ambako ndiko kwenye soko kubwa la dawa hii. Kiasi kikubwa cha heroin huingizwa Afrika kupitia nchi zilizoko katika ukanda wa pwani ya Mashariki kama Ethiopia, Kenya, Msumbiji na Tanzania. Kiasi kingine cha heroin huingizwa kupitia Bahari ya Hindi ikitokea Jamhuri ya Kiislamu ya Iran na Pakistan. Heroin pia huingizwa nchini Misri kutokea maeneo ya Kusini Mashariki na Kusini Magharibi mwa Asia. Kiwango kidogo cha heroin husafirishwa kutoka Afrika Mashariki kwenda Kusini mwa Afrika.

Heroin husafirishwa kwa kiasi kikubwa kupitia majini na kiasi kidogo cha dawa hiyo husafirishwa kwa njia ya anga. Mwezi Februari 2011, kilo 179 za heroin zilikamatwa Dar es Salaam, Tanzania na mwezi Machi mwaka huo kilo 102 za heroin zilikamatwa Mombasa, Kenya. Aidha, mwezi Januari 2012, kilikamatwa kiasi kikubwa cha kilo 211 za heroin mkoani Lindi ambacho hakijawahi kukamatwa katika nchi za Afrika Mashariki. Hivyo, katika kipindi kisichozidi miaka miwili takriban kilo 750 za heroin zilikamatwa katika ukanda wa pwani ya Afrika Mashariki.

Mwaka 2011 kiasi cha kilo 400 za heroin kilikamatwa katika nchi za Afrika Magharibi na kiasi cha kilo 113 za heroin zilikamatwa katika bandari ya Lagos huko Nigeria mwezi Juni 2012. Kuanzia Januari 2012 kumekuwepo na ukamataji wa heroin katika kiwanja cha ndege cha Abidjan huko Ivory Coast. Kiasi kikubwa cha heroin inayokamatwa Afrika Magharibi hupelekwa Benin, Ivory Coast na Nigeria. Heroin husafirishwa kutoka Afghanistan kwenda Afrika Kaskazini kupitia Ghuba ya Aqba nchini Misri. Ingawa kiasi kikubwa cha heroin hukusudiwa kupelekwa nje ya bara la Afrika, kumekuwa na ongezeko la kiasi kinachobakizwa kwa ajili ya matumizi barani humo.

Amfetamini, Saikotropiki na Kemikali Bashirifu

Dawa za kulevya aina ya amfetamini huzalishwa katika nchi za Kusini na Kaskazini mwa Afrika. Uzalishaji na usafirishaji wa Amfetamini kutoka Afrika Magharibi kwenda maeneo mengine umekuwa tishio katika kipindi cha hivi karibuni. Mwezi Julai 2011 huko Lagos, Nigeria maabara haramu, iliyokuwa na uwezo wa kutengeneza vidonge vyta metamfetamini kati ya kilo 20 hadi 50 kwa kila mzunguko wa uzalishaji iliharibiwa ambapo Mwezi Februari, 2012 iliharibiwa maabara haramu ya kutengeneza metamfetamini ikiwa na kilo 5 za dawa hiyo.

Hakuna taarifa zinazoonyesha kutengenezwa au kuzalishwa kwa amfetamini katika ukanda wa Afrika Mashariki ingawa kiasi cha kilo 5 za metamfetamini zilikamatwa huko Uganda mwaka 2012. Vilevile, nchini Tanzania mwaka 2009 hadi 2011 kumekuwepo na wizi wa jumla kilo 2,062 za *Pseudoephedrine* na kilo 1,183 za *ephedrine*.

Uzalishaji na utengenezaji wa metamfetamini, *metacathinone* na mandrax umeendelea kufanyika nchini Afrika Kusini. Dawa hizi huzalishwa kwa lengo la matumizi ya ndani ya nchi na kiasi kingine husafirishwa kwenda nchi nyingine za ukanda wa Kusini mwa Afrika. Katika kipindi cha mwaka 2012, vilikamatwa vidonge 860,000 ambavyo vinakaribia kilo 350 huko Afrika Kusini. Vidonge hivyo vilikuwa vinasafirishwa kwa njia ya barabara kwenda Jimbo la Cape nchini humo vikitokea Tanzania na Botswana. Vilevile, mwezi Julai 2012 ziliharibiwa maabara mbili haramu za kutengeneza mandrax zikiwa na vidonge 300,000 vyenye uzito wa kilo 120 jijini Johannesburg Afrika Kusini. Mwaka 2011 kilo 41 za ephedrini zilikamatwa nchini Msambiji na mwaka 2012 zilikamatwa kilo 1970 za 1-phenyl-2-propane (p-2-p) nchini humo zikitokea India. Aidha, zaidi ya tani 132 za tramadol zilikamatwa Afrika Magharibi katika kipindi cha Februari hadi Oktoba 2012, zikitokea India.

2.1.2 Matumizi na tiba

Kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa kukusanya takwimu za watumiaji wa dawa za kulevya katika nchi nyingi za Afrika limekuwa ni tatizo sugu linalochangia kuwepo kwa huduma hafifu za utoaji wa tiba. Matumizi ya bangi yameendelea kuzikabili nchi nyingi za Afrika ya Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambapo bangi iliyosindikwa hutumiwa zaidi katika nchi za Afrika ya Kaskazini. Kutokana na taarifa za UNODC², inakadiriwa kuwa kuna watumiaji takriban milioni 1.5 wa cocaine katika nchi za Afrika Magharibi na Afrika ya Kati ambayo ni sawa na asilimia kati ya 0.3 na 1.1 ya idadi ya watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 64. Nchi za Nigeria na Afrika Kusini ndizo zinazoongoza kwa utumiaji wa dawa hiyo. Hali hiyo

² (UNODC)

ni tofauti kwa nchi za Afrika Kaskazini na Afrika Mashariki ambako matumizi ya cocaine ni madogo.

Matumizi ya heroin yanaendelea kuongezeka hasa katika nchi za Afrika Mashariki na Afrika Magharibi. Heroin inayosafirishwa kwenda Afrika Magharibi na sehemu mbalimbali duniani hutokea Afrika Mashariki. Aidha, matumizi ya heroin kwa njia ya kujidunga yameongezeka sana katika eneo la Afrika Mashariki kuliko maeneo mengine ya Afrika hasa katika nchi za Tanzania na Kenya. Viwango vya utumiaji wa heroin nchini Mauritius ni asilimia 1.3, Kenya asilimia 0.7, Nigeria asilimia 0.7 na Afrika ya Kusini asilimia 0.5. Pia, heroin imekuwa ikitumiwa kwa kuchanganywa na cocaine na dawa nyingine za kulevya. Inakadiriwa kuwa nchini Kenya, kuna watumiaji zaidi ya 200,000 wa heroin mionganoni mwao 40,000 hadi 60,000 hutumia kwa njia ya kujidunga. Aidha, utumiaji wa amfetamini unakadiriwa kuwa asilimia 0.2 katika nchi za Afrika na unaongezeka mionganoni mwa watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 64. Nchi zinazoongoza kwa matumizi ya amfetamini ni Nigeria, Afrika Kusini na Misri.

Mirungi inayozalishwa kwa wingi nchini Kenya na Ethiopia hupelekwa Somalia na Yemen na nyingine barani Ulaya. Kutokana na athari za kifaya zinazoambatana na matumizi ya mirungi, nchi nyingi kama Tanzania, Rwanda, USA, Canada na nyingine za ulaya zimeharamisha mirungi. Aidha, matumizi ya Tramadol ambayo ni dawa hatari yameanza kujitokeza katika siku za hivi karibuni nchini Misri, Libya na Mauritius.

Katika kukabili ana na ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya, nchi za Afrika zimeanza kuchukua hatua mbali mbali ikiwemo utoaji wa tiba. Kwa mfano, nchini Tanzania kuna programu ya kutumia dawa aina ya methadone kutibu watumiaji wa heroin. Programu hii ilianza rasmi mwaka 2011 ambapo watumiaji wapatao 1,500 wanaendelea kupata huduma hii. Huduma ya methadone inatolewa pia katika nchi ya Mauritius.

2.2 Amerika

2.2.1 Amerika ya Kati na Caribbean

Eneo hili linaendelea kutumika kama sehemu maarufu ya kuitishia cocaine kuelekea Amerika Kaskazini. Aidha, miaka ya 2011 na 2012 kulikuwa na ongezeko la usafirishaji wa kemikali bashirifu kwenye nchi za Amerika ya Kati, hasa ambazo haziko kwenye orodha ya kemikali zinazodhibitiwa kimataifa.

2.2.1.1 Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji

Nakotiki³

Amerika ya Kati na Caribbean huzalisha bangi na kiasi kidogo cha afyuni. Mauaji mengi yanayotokea katika baadhi ya nchi za eneo hili huhusishwa na magenge yanayogombea udhibiti wa njia za kusafirisha dawa za kulevyu kuelekea Amerika ya Kaskazini. Mwezi Mei 2012, nchi ya Marekani ilikamata kilo 1,288 za cocaine kwenye boti iendayo kasi katika bahari ya kimataifa ya Caribbean. Wasafirishaji hutumia boti na nyambizi kusafirisha cocaine hadi Marekani. Jambo jipya kwenye eneo hili ni kuibuka kwa usafirishaji wa cocaine ya kimiminika.

Usafirishaji wa bangi, heroin na MDMA “ecstacy” umeripotiwa katika eneo hili na pia kumekuwa na uzalishaji wa afyuni hasa nchini Guatemala pamoja na ongezeko la usafirishaji wa dawa za tiba zenyenye madhara ya kulevyu nchini El – Salvador.

Saikotropiki⁴ –

Amfetamini pamoja na kemikali bashirifu za kutengeneza amfetamini zilikamatwa katika nchi mbalimbali za Amerika ya Kati na Caribbean hasa nchini Guatemala na Nicaragua ambapo maabara haramu za kutengeneza amfetamini zilikamatwa. Mchanganyiko wa dawa za tiba zenyenye madhara ya kulevyu kama vile *benzodiazepines, diazepines, alprazolam* na *donazepam* zilikamatwa katika maeneo haya.

Kemikali Bashirifu –

Inakadiriwa kuwa kilo 100 za *ephedrine*, kilo 95 za *pseudophedrine* na vidonge 530,310 vilikamatwa nchini Guatemala mwaka 2011 hadi 2012. Mwezi Januari 2012, kontena 12 za *mono-menthyl-amine* yenye uzito wa tani 195 zilikamatwa nchini Mexico. Kontena hizi zilitokea nchini China na 10 kati ya hizo zilielekezwu Guatemala na mbili nchini Nicaragua. *Mono-menthyl-amine* ni kemikali ambayo hutumika kutengeneza dawa ya kulevyu aina ya metamfetamini ingawa haiko kwenye orodha za kemikali zinazodhibitiwa kimataifa.

2.2.1.2 Matumizi na Tiba

Inakadiriwa kuwa matumizi ya cocaine kwa watu wa Amerika ya Kati kwa mwaka ni asilimia 0.5 na kwa watu wa Caribbean ni asilimia 0.7. Matumizi haya yanabaki

³ Nakotiki ni dawa za kulevyu ambazo huleta usingizi na uzubaifu kama Bangi, Cocaine na Heroin

⁴ Saikotropiki ni dawa za kulevyu zinazobadilisha hali za kisaikolojia na kusababisha mawazo na mtizamo wa mtumiaji.

kuwa juu kuliko wastani wa matumizi ya dunia kutokana na cocaine kusafirishwa kwa wingi kupitia maeneo haya. Vilevile, matumizi ya amfetamini yapo juu kuliko wastani wa matumizi ya dunia hasa katika nchi za El Salvador ambayo ni asilimia 3.3, Belize na Costa Rica ni asilimia 1.3 na Panama ni asilimia 1.2.

Kutokana na taarifa ya UNODC inakadiriwa kuwa kuna watumiaji wa amfetamini ukiondoa “ecstacy” wapatao 330,000 huko Amerika ya Kati na watu 220,000 huko Caribbean. Matumizi ya bangi kwa mwaka yanakadiriwa kuwa asilimia 2.4 kwa Amerika ya Kati na asilimia 2.8 kwa Caribbean, wakati matumizi ya afyuni ni asilimia 0.5 kwa Amerika ya Kati na asilimia 0.4 kwa Caribbean. Nchi za El Salvador, Honduras, Nicaragua, Panama na Cuba zina programu mbalimbali za kinga na tiba pamoja na elimu na mafunzo kwa watendaji na makundi tofauti kama vile wazazi na wanataaluma.

2.2.2 Amerika Kaskazini

Amerika Kaskazini inabakia kuwa soko kuu la aina mbalimbali za dawa za kulevyu duniani ingawa matumizi ya baadhi ya dawa hizo yamepungua. Wafanyabiashara haramu wa dawa za kulevyu kwenye eneo hili wameendelea kutengeneza dawa mpya za kulevyu ambazo haziko kwenye orodha ya dawa zinazodhibitiwa kisheria. Pia, eneo hili limekuwa na vifo vingi vinavyohusiana na biashara na matumizi ya dawa hizo kama ilivyo katika maeneo mengine.

2.2.2.1 Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji

Mitandao ya wafanyabiashara haramu wa dawa za kulevyu imeendelea kugundua mbinu mbalimbali za usafirishaji wa dawa za kulevyu zikiwemo kutumia nyambizi kwenye eneo hili. Vile vile, ujenzi wa njia za kisasa chini ya ardhi kwa ajili ya kusafirisha dawa hizo kwenda nchi nyingine umeendelea. Njia zaidi ya 150 ziligungnduliwa nchini Marekani tangu mwaka 1990, hali iliyosababisha tani nyingi za dawa za kulevyu hasa bangi kukamatwa.

Nakotiki

Bangi inaendelea kuzalishwa na kusafirishwa kwa wingi katika nchi zote tatu zilizopo eneo hili. Uzalishaji wa bangi mashambani umeendelea kuwepo ambapo Marekani imegundua ulimaji kwenye misitu ya nchi hiyo. Pia, uzalishaji wa bangi majumbani umeendelea hasa nchini Marekani na Canada. Kilimo cha afyuni nchini Mexico kiliongezeka ambapo kiasi cha tani 1.45 kilikamatwa mwaka 2011 ikiwa ni tani moja zaidi ya kilichokamatwa mwaka 2010. Heroin zaidi ya kilo 685 zilikamatwa mwaka 2011 nchini Mexico, lita 3,640 za heroin ya kimiminika nazo zilikamatwa nchini humo ukiwa ni ukamataji mkubwa zaidi kuwahi kutokea. Aidha, kiasi kikubwa cha heroin inayotumiwa nchini marekani hutokea kwenye nchi za Mexico na Colombia.

Usafirishaji wa cocaine katika eneo hili ulipungua kutokana na kudhibitiwa kwa njia ya kusafirisha dawa hii kupitia Mexico, kupungua uzalishaji kwa asilimia 47 nchini Colombia na kuwepo vurugu kati ya magenge haramu nchini Mexico. Kupungua kwa upatikanaji wa cocaine kumeongeza bei na kusababisha wafanyabiashara kuchanganya dawa hiyo na vitu vingine ili kuongeza kiwango na kupunguza ubora wa dawa hiyo mitaani.

Udhibiti wa dawa za tiba zenyе madhara ya kulevyя hasa zenyе asili ya afyuni umeendelea kuwa changamoto kubwa kwa watendaji wa vyombo vya udhibiti katika eneo hili. Kuna uchepushwaji mkubwa wa dawa hizi pamoja na utengenezaji bandia wa dawa za tiba zenyе madhara ya kulevyя. Zaidi ya vidonge milioni 3 vilichepushwa nchini Canada kati ya mwaka 2009 na 2011.

Saikotropiki

Uzalishaji wa metamfetamini nchini Mexico uliendelea kuongezeka na kusababisha bei kupungua na kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa hiyo nchini Marekani. Ongezeko la upatikanaji wa metamfetamini lilichangiwa na kujitokeza kwa njia mpya na rahisi za utengenezaji wa dawa hizi. Taarifa iliyotolewa na nchi ya Mexico pamoja na Marekani inaonyesha kuwa kulikuwa na ongezeko la asilimia 1,000 la ukamataji wa maabara haramu za utengenezaji wa metamfetamini kati ya mwaka 2010 hadi 2011. Aidha, taarifa zinaonesha kuwa, Canada imebakia kuwa chanzo kikuu cha dawa ya kulevyя aina ya “ecstasy” nchini Marekani.

Kemikali bashirifu

Zaidi ya miaka 10 iliyopita Serikali za Amerika ya Kaskazini zimeimarisha hatua za udhibiti na kuongeza juhudи za kuzuia uchepushaji wa kemikali bashirifu. Aidha, kemikali zinazotumika kutengeneza dawa za tiba zenyе madhara ya kulevyя huchepushwa na kutengeneza dawa za kulevyя kama vile “esters” zinazotokana na “phenyl-acetic acid”.

Dawa mpya za kulevyя zinazozidi kugunduliwa

Watengenezaji wa dawa za kulevyя wa Amerika Kaskazini waliendelea kugundua dawa mpya za kulevyя zenyе kemikali ambazo hazizuiwi na sheria zilizopo sasa. Utengenezaji wa dawa mpya kama vile “spice”, “plant food”, “bath salts” na “legal highs” ambazo zikitumiwa huleta matokeo kama yale ya matumizi ya bangi, “ecstasy” na amfetamini uliongezeka. Halikadhalika, nchini Mexico uligundulika mmea wenye kemikali inayolevya isiyodhibitiwa kisheria ambaо hutumiwa na baadhi ya makabila kwenye sherehe za kidini.

2.2.2.2 Matumizi na Tiba

Amerika ya Kaskazini inaongoza kwa matumizi ya bangi, heroin na cocaine kuliko maeneo mengine duniani. Vile vile, dawa za tiba zenyenye madhara ya kulevy ya hutumiwa zaidi kuliko heroin. Hata hivyo, matumizi ya dawa za tiba zenyenye madhara ya kulevy ya amfetamini yamepungua nchini Marekani. Aidha, taarifa zilizotolewa Mwezi Juni 2012 nchini Marekani zinaonesha ongezeko la watu wenye uraibu wa dawa nyingine za kulevy zisizo na asili ya afyuni. Kuanzia mwaka 1997 hadi 2010 idadi ya watumiaji wenye uraibu wa dawa za kulevy za jamii ya afyuni iliongezeka kutoka asilimia moja hadi asilimia 8.6, kiwango ambacho ni kikubwa zaidi ya watumiaji wa cocaine na amfetamini. Mahitaji ya tiba kwa uraibu wa bangi yaliongezeka kutoka asilimia 16 mwaka 2007 hadi asilimia 18.4 mwaka 2010.

2.2.3 Amerika ya Kusini

Eneo hili limeathirika na kilimo haramu cha mimea ya coca, baruti-afyuni (opium poppy) na bangi. Pia, upo utengenezaji na uzalishaji wa cocaine, heroin na bangi zinazotokana na kilimo hicho, hivyo matumizi ya dawa hizi yanayoongezeka.

2.2.3.1 Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji

Nakotiki

Kumekuwa na ongezeko la ukamataji wa bangi katika miaka ya karibuni kwenye nchi nyingi za Amerika ya Kati hasa nchini Bolivia. Nchini Brazil ukamataji uliongezeka kwa asiliami 12 kutoka tani 155 mwaka 2010 hadi tani 174 mwaka 2011. Kiasi kikubwa cha bangi iliyokamatwa ilitokea nchini Paraguay ingawa bangi nyingine ilikamatwa katika nchi za Colombia, Chile, Ecuador na Bolivia . Serikali ya Bolivia imeanzisha mkakati wa kupunguza kilimo cha coca kwa kupunguza eneo linaloruhusiwa kulima zao hili, ung'oaji wa hiari wa mimea hiyo pamoja na uteketezaji wake. Kilimo cha coca kiliongezeka nchini Colombia mwaka 2011 hadi kufikia hekta 64,000 kulinganisha na hekta 62,000 zilizolimwa mwaka 2010. Mamlaka za nchi hiyo ziliteketeza hekta 34,170 za coca na hekta 103,302 za mimea ya coca zilimwagiwa sumu.

Ukamataji wa cocaine ulipungua mwaka 2011 katika nchi nyingi zikiwemo Brazil, Colombia, Peru na Uruguay. Nchi zilizoongeza ukamataji ni Bolivia, Ecuador na Venezuela wakati Chile na Paraguay ukamataji haukubadilika. Kama ilivyo kwenye maeneo mengine ya Bara la Amerika cocaine husafirishwa kwa kutumia nyambizi. Aidha, afyuni hulimwa kwa kiwango kidogo kwenye eneo hili japokuwa nchi za Colombia, Ecuador na Peru ziliteteketeza mimea hiyo. Heroin inayozalishwa Colombia hupelekwa Ulaya, Mexico na Marekani.

Saikotropiki

Katika eneo hili la Amerika ya Kusini kumekuwepo matumizi ya dawa za kulevyta na zile za tiba zenye madhara ya kulevyta. Taarifa iliyotolewa mwaka 2011 inaonesha kuwa wanafunzi wa sekondari katika nchi za Bolivia, Colombia na Paraguay ni mionganoni mwa watumiaji wa dawa za kulevyta. Matumizi ya dawa za viwandani yanaweza kuhuishwa na ukamataji wa amfetamini kwenye nchi za Argentina, Brazil, Chile, Colombia, Ecuador na Uruguay mwaka 2011.

Kemikali bashirifu

Tindikali aina ya *Sulphuric* na *hydrochloric* zimekamatwa kwa wingi katika nchi za Colombia, Bolivia na Peru ambazo huzalisha cocaine . Kati ya mwaka 2005 hadi 2011 nchi hizo zilikamata takriban asilimia 40 ya tindikali hizo zilizokamatwa duniani kote. Nchini Colombia, watengenezaji wa cocaine hurudia kuzitumia kemikali bashirifu zilizokwishatumiwa kutengeneza cocaine ili kutengeneza cocaine mpya kwa lengo la kupunguza hatari ya kugundulika na kupunguza ghamraza za utengenezaji. Kemikali ya *Potassium permanganate* ambayo hutumika katika uzalishaji wa cocaine nayo imeendelea kuwa tatizo kubwa katika nchi za eneo hilo.

2.2.3.2 Matumizi na Tiba

Kutokana na taarifa zilizotolewa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia masuala ya Uhali na Dawa za Kulevyta (UNODC) pamoja na Serikali za nchi za Amerika ya Kusini matumizi ya bangi ni makubwa katika nchi za Uruguay kwa asilimia 8.3, Chile asilimia 4.9, Bolivia asilimia 4.5 na Suriname asilimia 4.3. Matumizi hayo ni makubwa zaidi mionganoni mwa vijana. Kwa mfano, viwango vya utumiaji nchini Chile mionganoni mwa vijana wa umri kati ya miaka 15 hadi 16 ni asilimia 16.2 na nchini Uruguay matumizi ni asilimia 12.5 kwa vijana wenye umri kati ya miaka 13 hadi 17 . Nchi nyingine ambazo bangi hutumika ni Brazil na Colombia.

Taarifa ya UNODC, inaonesha kuwa matumizi ya cocaine Amerika ya Kusini kwa mwaka 2010 yalibakia kuwa asilimia 0.7. Nchini Brazil inakadiriwa kuwa matumizi ya cocaine mionganoni mwa watu wazima ni asilimia 2. Japokuwa kumeripotiwa kupungua matumizi ya cocaine kwenye baadhi ya nchi za eneo hili zikiwemo Argentina na Chile, mahitaji ya tiba mionganoni mwa watumiaji wa cocaine ni makubwa kuliko watumiaji wa aina nyingine ya dawa za kulevyta. Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2008, nchi iliyokuwa na viwango vidogo kabisa vya matumizi ya dawa za kulevyta ilikuwa ni Colombia kwa asilimia 0.02. Mwaka 2007, viwango vikubwa vya matumizi nchini Bolivia vilikuwa asilimia 0.6. Aidha, matumizi ya dawa za kulevyta za viwandani mionganoni mwa vijana yanaongezeka. Kwa mfano; Serikali za nchi za Argentina, Chile na Colombia zimeripoti matumizi ya MDMA

(“ecstasy”) katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Pia, kuna tatizo la matumizi ya viyeyushi kama petroli na gundi hasa mionganoni mwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu katika nchi za Amerika ya Kati, Kusini na Caribbean.

2.3 Ulaya

2.3.1 Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji

Nakotiki

Kilimo cha bangi katika nchi za Ulaya Magharibi na Ulaya ya Kati hasa kilimo cha bangi ya majumbani kwa ajili ya biashara kimeendelea kuongezeka. Aidha, kumekuwepo na makundi ya uhalifu yanayojihuisha na kilimo cha bangi katika nchi za Bulgaria, Denmark , Ujerumani, Italia, Ufaransa, Norway, Slovakia, Sweden na Uingereza.

Tafiti zinaonyesha kuwa nchi 16 kati ya nchi 30 zilizopo Ulaya, zinajihuisha na kilimo cha bangi ya majumbani. Nchi za Czech na Ufaransa zinaongoza kwa uzalishaji wa bangi ya majumbani ambapo robo tatu ya bangi yote inayozalishwa katika nchi hizi inatokana na kilimo cha aina hiyo. Usafirishaji wa bangi katika nchi za Ulaya umeendelea kwa kiwango kikubwa katika maeneo ya Ulaya Mashariki na Ulaya ya Kati. Bangi inayosafirishwa kwenda Montenegro na Bosnia-Hezegovina hutokea katika nchi za Yugoslavia ya zamani, Macedonia, Albania na Kosovo. Kumekuwepo na ukamataji wa kiwango kidogo cha bangi inayozalishwa nchini Albania, ambapo uzalishaji umeongezeka katika nchi za Bulgaria na Ukraine.

Katika kipindi cha mwaka 2011, kesi 89 za uzalishaji bangi ziliripotiwa na mimea 21,267 ya bangi iliharibiwa ambapo watu 79 walikamatwa na kuwekwa chini ya uchunguzi maalum kwa ajili ya kufunguliwa mashtaka ya uzalishaji wa bangi.

Ukamataji wa bangi iliyosindikwa inayoingizwa katika Bara la Ulaya umeendelea kupungua ukilinganisha na kipindi cha miaka kumi iliyopita. Ukamataji kwa kiasi kidogo cha bangi iliyosindikwa mwaka 2010 umejitokeza katika nchi ya Hispania ambayo huongoza kwa kukamata aina hii ya bangi. Kwa ujumla ukamataji wa bangi iliyosindikwa ulipungua kutoka tani 178 mwaka 2010 hadi tani 147 mwaka 2011. Kiasi kikubwa cha Bangi iliyosindikwa kinachokamatwa Ulaya hutokea Afrika Kaskazini, hasa nchini Morocco.

Cocaine

Ukamataji wa Cocaine katika nchi za Ulaya Magharibi na Ulaya ya Kati umepungua katika miaka ya hivi, ingawa ukamataji wa dawa hii uliongezeka kutoka tani 50 mwaka 2009 hadi tani 60 mwaka 2010, ukamataji wa cocaine ulibakia kuwa nusu ya ule uliofanyika mwaka 2006 wa tani 120. Nchi ya Hispania imeendelea

kuongoza kwa ukamataji wa kiasi kikubwa cha cocaine uliofikia tani 25 ambayo ni nusu ya kiasi chote cha dawa hiyo kilichokamatwa katika eneo la Ulaya Magharibi na Ulaya ya Kati, ikifuatiwa na Uholanzi iliyokamata tani 10.

Cocaine husafirishwa kupitia bandari zilizoko nchini Croatia na Ugiriki hadi Ulaya Mashariki. Kutoka huko, cocaine hupelekwa katika bandari ndogo za Montenegro na Albania na baadaye hupelekwa Kosovo na Serbia kabla ya kufika Bosnia na Hezegovina na kwenye masoko ya Ulaya Magharibi.

Saikotropiki

Dawa za kulevya aina ya amfetamini zilizokamatwa Ulaya Magharibi mwaka 2011 zilikuwa kilo 1,827 kiasi ambacho ni mara tatu zaidi ya kilo 615 zilizokamatwa mwaka 2010, ingawa kiasi kilichokamtwa mwaka 2011 kilikuwa kidogo kikilinganishwa na kilo 3,028 zilizokamatwa mwaka 2009. Ulaya imeendelea kuongoza kwa kukamata maabara haramu za kutengeneza dawa za kulevya duniani ambapo mwaka 2009 zilikamatwa maabara 43 na mwaka 2010 zilikamatwa maabara 62.

Uzalishaji wa metamfetamini uliongezeka katika nchi za Nordic na Baltic ingawa dawa hizi hazitumiwi kwa wingi huko Ulaya. Idadi ya maabara za kutengeneza metamfetamini katika nchi za Ulaya imepungua kutoka 361 mwaka 2009 hadi 328 kwa mwaka 2010. Nyingi ya maabara hizo yaani 307 zilikamatwa huko Jamhuri ya Czeck ikifuatiwa na Austria na Bulgaria.

Kemikali bashirifu

Kuna tatizo la kemikali bashirifu mpya zinazoendelea kugunduliwa na mitandao ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Tatizo hili lilikuwa dogo kabla ya mwaka 2010 hata hivyo, kulikuwa na ukamataji mkubwa wa kemikali za aina ya alpha – phenyl katika miaka ya 2009 na 2011.

Dawa mpya za kulevya zinazozidi kugunduliwa

Tatizo la kuzalisha, kusafirisha na kutumiwa kwa dawa mpya zinazoendelea kugunduliwa limeendelea kuwa kubwa katika nchi za Ulaya Magharibi na Ulaya ya Kati. Kiasi kikubwa cha dawa za aina hii kilihusisha aina 23 za *synthetic cannabinoids* na 8 za *synthetic cathinones*.

2.3.2 Matumizi

Tafiti zinaonyesha kuwepo kwa ongezeko la matumizi ya bangi na aina ya amfetamini ikiwemo “Ecstasy” katika maeneo ya Mashariki na Kusini Mashariki mwa Ulaya ambapo matumizi ya cocaine na opioids katika nchi mbalimbali za Ulaya Magharibi na Kati hayakubadilika. Hata hivyo, matumizi ya dawa hii yalipungua mionganoni mwa watu wazima kwenye nchi za Hispania, Ireland, Denmark na Uingereza.

Wastani wa matumizi ya bangi Ulaya Mashariki na Kusini Mashariki yanakadiriwa kufikia asilimia 2.6 ya watu wote katika maeneo hayo ambapo matumizi ya opioids ni asilimia 1.2 na opiates ni asilimia 0.8. Matumizi ya Cocaine yanakadiriwa kuwa ya wastani wa kati ya asilimia 0.1 na 0.3 ya idadi ya watu wote wa Kusini Mashariki mwa Ulaya. Matumizi ya amfetamini ni kati ya asilimia 0.5 na matumizi ya "ecstacy" ni kati ya asilimia 0.5 na 0.6 ya watu wote Kusini Mashariki mwa Ulaya.

2.4 Asia

2.4.1 Mashariki na Kusini Mashariki

Eneo hili limeendelea kuwa la pili duniani kwa uzalishaji wa baruti-afyuni (opium poppy) hasa katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao na Myanmar ambazo zimeripoti ongezeko la uzalishaji kwa miaka sita mfululizo kutoka mwaka 2007 hadi 2012. Kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji la takriban asilimia 66 kwa nchi ya Lao na asilimia 17 kwa nchi ya Myanmar kuanzia mwaka 2011 hadi 2012. Eneo hili linaendelea kuwa kitovu cha utengenezaji wa amfetamini na soko la metamfetamini. Usafirishaji na matumizi ya dawa za tiba zenye madhara ya kulevya ni tatizo kubwa kwenye maeneo haya.

2.4.1.1 Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji

Kutokana na kushamiri kwa kilimo cha *opium poppy* katika eneo hili, nchi za Lao, Myanmar na Thailand zilifanya uteketezaji wa mashamba ya *opium poppy* (baruti-afyuni). Nchi ya Lao iliteketeza hekta 700 na Myanmar iliteketeza hekta 23,700 mwaka 2012.

Kilimo cha bangi na ukamataji wa dawa hiyo viliendelea kuripotiva kwenye nchi za Indonesia na Ufilipino ambazo huzalisha bangi kwa wingi katika eneo hili. Kiasi kidogo cha bangi iliyosindikwa huingizwa nchini Indonesia ikitokea nchi za Denmark na Ufaransa. Nchi nyingine zilizokamata bangi ni Cambodia, China, Japan, Lao, Myanmar, Jamhuri ya Korea na Thailand.

Kiasi cha zaidi ya tani 7 za heroin kilikamatwa nchini China mwaka 2011 na kilo 12 zilikamatwa nchini Lao mwaka 2012. Kiasi kikubwa cha heroin kilichokamatwa kilitokea eneo linalojulikana kama Golden Triangle. Ukamataji wa cocaine mwaka 2011 ulipungua ingawa, mwezi Julai 2012, kulikuwa na ukamataji wa kilo 650 za cocaine ndani ya kontena huko Hong Kong nchini China lililokuwa likisafirishwa kwa meli kutoka Ecuador.

Saikotropiki

Ukamataji wa metamfetamini kwenye maeneo ya Mashariki na Kusini Mashariki mwa Asia uliendelea kuongezeka mwaka 2011 hasa katika nchi za China na

Thailand. Katika kipindi cha miezi 8 ya mwaka 2012, vilikamatwa vidonge milioni 50.8 vya metamfetamini na kilo 870 za *crystalline* metamfetamini nchini Thailand. Kiasi kikubwa cha amfetamini kilichokamatwa kilizalishwa katika nchi za eneo hilo. Maabara haramu zipatazo 357 ziliharibiwa nchini China mwaka 2011 nyingi kati ya hizo zilikuwa zikizalisha metamfetamini na *ketamine*. Mwaka huo wa 2011 nchi ya Indonesia iliharibu maabara 6 na Ufilipino maabara 14. Myanmar inabaki kuwa msambazaji mkuu wa amfetamini kwenye nchi za China, Lao na Thailand na kutoka nchi hizo dawa hiyo husafirishwa hadi Cambodia na Vietnam.

Kemikali bashirifu

Changamoto kubwa katika eneo hili ni udhibiti wa usafrishaji wa kemikali bashirifu aina ya *ephedrine* na *pseudophedrine* ambazo huweza kutumika kutengeneza amfetamini. Kuimarishwa kwa udhibiti wa kemikali bashirifu kumesababisha wasafirishaji kubadili mwelekeo na kwenda nchi zisizo na udhibiti mkali kama vile Jamhuri ya Korea ambapo Desemba 2011 vidonge milioni 2 vilikamatwa nchini Thailand vikitokea nchini humo. Mwezi Aprili 2012, operesheni ya pamoja kati ya Australia na China ilivuruga mpango wa genge la kimataifa liliodhamiria kusafirisha jumla ya tani 3.4 za kemikali aina ya “safrole-rich oil” kutoka China hadi Australia.

Dawa mpya za kulevyaa zinazozidi kugunduliwa

Ketamine ni dawa ya tiba yenye madhara ya kulevyaa ambayo inatumika isivyo halali katika eneo hili. China ikiwemo Hong Kong ilikamata tani 5.7 za ketamine mwaka 2011 kiasi ambacho ni kikubwa kuwahi kukamatwa katika eneo hilo. Vilevile, kumeibuka dawa mpya za kulevyaa katika eneo hili ambapo Jamhuri ya Korea imeripoti kukamatwa kwa bidhaa zinazouzwa kama viungo na chumvi zinazotumika kama mbadala wa cocaine au “ecstasy”.

2.4.1.2 Matumizi na Tiba

Heroin hutumiwa kwa wingi katika nchi za China, Malaysia, Myanmar, Singapore na Vietnam. Nchini China kulikuwa na watumiaji wa heroin wapatao milioni 1.2 mwaka 2011 ikiwa ni asilimia 64 ya watumiaji wote. Asilimia 87 ya watu waliotibwa kwa matumizi ya dawa za kulevyaa nchini Myanmar walitumia heroin. Nchi nyingi za eneo hili zimeripoti hali ya matumizi ya heroin kutobadilika au kupungua.

Bangi imeendelea kuwa dawa inayotumiwa na watu wengi nchini Indonesia hasa kutokana na kupatikana kwa wingi nchini humo. Pia, ni ya pili kwa kutumiwa katika nchi za Japan, Ufilipino, Jamhuri ya Korea na Thailand na ya tatu katika nchi za Malaysia na Myanmar. Vilevile, kuna matumizi ya amfetamini katika nchi nyingi za bara la Asia hasa aina ya metamfetamini. Changamoto kubwa ni kuwepo kwa ongezeko la vijana wanaotumia dawa za kulevyaa. Asilimia 70 ya watu walio chini

ya umri wa miaka 35 walitumia dawa za *synthetic* nchini China. Matumizi ya dawa za kulevyta kwa njia ya kujidunga yameripotiwa katika nchi nyingi. Nchini China watumiaji wa dawa za kulevyta hulazimishwa kupata tiba kwenye vituo vya tiba. Mwishoni mwa mwaka 2011, zaidi ya watu 220,000 waliendelea kupatiwa tiba vituoni. Pia watu wapatao 97,000 walikuwa wakitibwa katika vituo vya kijamii na vya utengemao.

2.4.2 Asia Kusini

Kwa ujumla eneo hili limeendelea kukabiliwa na tatizo la uchepushwaji wa dawa za tiba zenye madhara ya kulevyta pamoja na matumizi holela ya dawa hizi.

2.4.2.1 Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji

Nakotiki

Dawa za tiba zenye madhara ya kulevyta zimeendelea kuchepushwa kutoka nchini India. Nchi hiyo imebakia kuwa chanzo kikuu cha dawa hizo zinazosafirishwa kwenda katika nchi nyingine za eneo hilo na nyinginez duniani. Kiasi kikubwa cha dawa hizo kinachoche pushwa ni za aina ya *codeine*, *dextropropoxyphene* na *pethidine*. Kiasi kikubwa cha dawa za nakotiki kutoka India huingizwa nchini Bangladesh, Bhutan na Nepal. Aidha, dawa hizo kutoka India hupitia Pakistan, Srilanka hadi Maldives.

Bangi na *opium poppy* hulimwa nchini India na kilimo cha *opium poppy* hufanyika katika nchi za Nepal na Bangladesh. Heroin kutoka Afghanistan imeanza kuuzwa nchini Bangladesh hivi karibuni ambayo huingizwa nchini humo kupitia misituni, milimani na baharini. Kiwanja cha ndege kilichopo Dhakar na Bandari ya Chittagong hutumika kusafirisha heroin.

Saikotropiki

Kama ilivyo kwa dawa za nakotiki, dawa za saikotropiki nazo zimeendelea kuchepushwa nchini India na kupelekwa nchi jirani hasa Bangladesh, Bhutan, Nepal na kwingineko. Dawa za saikotropiki zinazoche pushwa zaidi ni *benzodiazepines* na *buprenorphine*.

Usafirishaji wa Amfetamini hasa vidonge vya metamfetamini kutoka Myanmar hadi Asia Kusini unaendelea kuongezeka kwa mfano; nchini Bangladesh ukamatataji uliongezeka kwa kiwango cha juu mwaka 2011 ambapo vidonge milioni 1.4 vilikamatwa ukilinganisha na vidonge 800,000 vilivyokamatwa mwaka 2012. Halikadhalika, zilikamatwa kilo 473 za amfetamini nchini India mwaka 2011. Vilevile, kilo 72 za Mandrax (methaqualone) zilikamatwa mwaka 2011 nchini India ingawa hakuna maabara haramu ya uzalishaji wa dawa hiyo uliowahi kukamatwa nchini humo tangu 2009.

Kemikali bashirifu

Nchi za Asia Kusini zimeendelea kuwa chanzo cha uzalishaji wa kemikali bashirifu. Magenge ya wahalifu wa dawa za kulevyta husafirisha kemikali hizi hasa *ephedrine* na *pseudoephedrine* kwa ajili ya kutengeneza amfetamini. Kwa mfano, mamlaka za udhibiti nchini India zilikamata kiasi cha tani 7.2 mwaka 2011 na tani 2.3 za kemikali hizo katika kipindi cha miezi 6 ya mwanzo wa mwaka 2012. Hili ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na kipindi cha kuanzia mwaka 2008 hadi 2010. Kuanzia mwezi Novemba 2011 hadi mwishoni mwa mwezi Juni 2012, vidonge milioni 30 vya *pseudoephedrine* vilivyokuwa vikisafirishwa kwenda Mynamar vilikamatwa nchini India. Aidha, ukamataji wa *acetic anhydride* nchini India ulipungua kutoka mwaka 2008 ambapo tani 2.8 za kemikali hiyo zilikamatwa na hakuna kiasi chochote kilichokamatwa mwaka 2011.

Dawa mpya za kulevyta zinazozidi kugunduliwa

Mwaka 2011 nchi ya India iliingiza kemikali aina ya *ketamine* katika orodha ya kemikali inayodhibitiwa katika sheria zake za udhibiti wa dawa za kulevyta. Kiasi cha dawa aina ya *ketamine* kilichokamatwa nchini India kimeongezeka kutoka tani 1.3 mwaka 2010 hadi tani 1.5 mwaka 2011. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2012 kiasi cha tani 350 za *ketamine* kilikamatwa nchini humo.

2.4.2.2 Matumizi na Tiba

Inakadiriwa kuwa watumiaji wa bangi Asia Kusini ni asilimia 3.6 na watumiaji wa opiods ni asilimia 0.3. Bangi hutumiwa kwa wingi nchini India ikifuatiwa na dawa za kulevyta za jamii ya opiods. Vilevile, dawa aina ya *benzodiazepines* hutumiwa kwa kiwango kikubwa katika eneo hili. Dawa za kutibu kifua zenye "Codeine" hutumiwa kwa wingi nchini India na Bangladesh. Katika kipindi cha mwaka 2010, nchini India asilimia 22 ya watumiaji wa dawa za kulevyta waliopatiwa tiba walitumia bangi, asilimia 66 walitumia opiods, asilimia 33 heroin na asilimia 19 walitumia dawa za tiba za jamii ya *opioids*.

Katika kipindi cha mwaka 2012 India ilianzisha huduma ya kutibu wajidunga kwa kutumia dawa aina ya methadone ambapo wajidunga 250 walihudumiwa. Aidha, inakadiriwa kuwa watu wapatao 30,000 hadi 34,000 wanatumia dawa za kulevyta kwa njia ya kujidunga huko Nepal. Nchini Srilanka takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2010 kulikuwa na matumizi makubwa ya bangi ikifuatiwa na *opiates* ambapo asilimia 1.4 ya watu wote wenye umri kati ya miaka 15 hadi 64 walitumia dawa hizo. Watumiaji wa dawa za kulevyta nchini Srilanka wanafikia 245,000 ambapo 200,000 wanatumia bangi na kiasi kilichobaki hutumia heroin.

2.4.3 Asia Magharibi

2.4.3.1 Uzalishaji na Usafirishaji

Taarifa zinaonesha kuwa katika mwaka 2012, kilimo cha *opium poppy* kilifikia hekta 154,000 nchini Afghanistan, ikiwa ni ongezeko la asilimia 18 ikilinganishwa na mwaka 2011. Kiasi hicho ni asilimia 64 ya kilimo chote cha *opium poppy* duniani.

Kilimo cha *opium poppy*, kiliongezeka nchini Afghanistan katika jimbo la Helmand. Hata hivyo, kilimo hicho kiliendelea katika majimbo ya Kati na Mashariki mwa nchi hiyo pamoja na jimbo la Kandahar. Nchini Afghanistan idadi ya majimbo maarufu kwa kilimo cha *opium poppy* ni 17, ambayo yana hekta zaidi ya 100 kwa kila jimbo katika mwaka 2012. Afghanistan huzalisha zaidi ya robo tatu ya heroin yote duniani ingawa uzalishaji huo ulipungua kwa tani 3,700 ikilinganishwa na tani 5,800 zilizozalishwa mwaka 2011.

Mwezi Agosti 2012, jumla ya hekta 9,672 za *opium poppy* ziliteketezwa katika majimbo 18 nchini Afghanistan, ambalo ni ongezeko la asilimia 154 ukilinganisha na kiasi kilichoteketezwa mwaka 2011. Wakulima pamoja na watumiaji hupambana na vyombo vya dola wakati wa uteketezaji wa mashamba ya *opium poppy*. Katika kipindi cha mwezi Juni mwaka 2012 jumla ya watu 102 walifariki dunia kutokana na mapambano hayo na wengine 127 walijeruhiwa.

Miongoni mwa nchi zinazoongoza duniani kwa uzalishaji wa bangi, tano zinatoka katika eneo la Asia Magharibi zikiwemo Afghanistan, Lebanon na Pakistani. Kwa mfano, nchini Afghanistan katika kipindi cha mwaka 2011 eneo lilolimwa bangi lilikuwa hekta 8,000 hadi 17,000 na uzalishaji ulifikia kiasi cha tani 1,000 hadi 1,900.

Saikotropiki

Kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji, usafirishaji na ukamataji wa dawa za kulevy aina ya amfetamini. Pia, utengenezaji na usafirishaji pamoja na matumizi ya metamfetamini viliendelea kuwepo. Jamhuri ya Kiislamu ya Iran ilikamata tani 3.9 za metamfetamini kiasi ambacho ni mara tatu zaidi ya kiasi kilichokamatwa hapo awali. Nchi ya Saudi Arabia imeendelea kuwa soko la dawa za kulevy za amfetamini pamoja na dawa bandia za tiba zinazotengenezwu nchini humo na zingine husafirishwa kwenda Syria na Jordan.

Kemikali bashirifu

Serikali ya Jordan ilizua uingizaji wa kemikali bashirifu aina ya *P-2-P* kuanzia mwezi Mei mwaka 2012. Kabla ya hapo nchi hii ilikuwa inaongoza duniani kwa uingizaji wa kiasi kikubwa cha kemikali hizo, ambazo zilitumika nchini humo na

nyingine zilisafirishwa kwenda nchini Iraq. Vile vile, Jordan imekuwa ikipambana na uchepushwaji wa kemikali bashirifu zinazotengeneza amfetamini na vidonge bandia vya *captagon*.

Tatizo la uingizwaji wa kemikali za *ephedrine* na *pseudoephedrine* limeendelea kuzikumba nchi nyingi za Asia Magharibi. Kemikali za *pseudoephedrine* huingizwa kwa kiwango kikubwa katika nchi za Iran, Syria na Pakistan hivyo kuongeza uwezekano wa uchepushwaji wa kemikali hizo. Tangu mwezi Machi 2012 kiwango kikubwa cha uchepushwaji wa *ephedrine* kimesababisha kuimariswa kwa shughuli za udhibiti nchini humo.

Dawa Mpya za Kulevya zinazozidi kugunduliwa

Dawa za kulevya zisizodhibitiwa kimataifa katika eneo hili zimeendelea kukamatwa. Mwaka 2011 jumla ya kilo 25 za mirungi zilikamatwa nchini Saudi Arabia zikitokea Yemen. Vile vile, matumizi ya mirungi yameripotiwa nchini Israel. Aidha, viyeyushi na vichangamushi vinatumwa kwa wingi katika nchi za Saudi Arabia na Israel.

2.4.3.2 Matumizi na Tiba

Dawa za kulevya aina ya *opiates* hutumiwa kwa wingi zaidi katika nchi nyingi za Asia Magharibi. Matumizi ya heroin katika nchi ya Afghastan na jirani zake yapo kwa kiwango cha juu. Vile vile, taarifa zinaonyesha kuwepo kwa watumiaji kwa njia ya kujidunga katika nchi za Mashariki ya Kati na inakadiriwa kuwa kuna wajidunga 20,000 nchini Afghanistan na 2,000 hadi 4,000 nchini Lebanon. Aidha, katika Jamhuri ya Kiislamu ya Iran asilimia 18.7 ya watu wapatao milioni 1.5 ni wajidunga. Huduma za matibabu katika nchi za ukanda huu, ni kwa waathirika waliotumia dawa za kulevya aina ya heroin. Afghanistan ina uwezo mdogo wa kutibu watumiaji ambao ni asilimia 3 tu ya watumiaji wote wanaotibiwa.

2.5 Oceania

2.5.1 Uzalishaji, Utengenezaji na Usafirishaji

Nakotiki

Bangi imeendelea kuwa dawa ya kulevya inayolimwa, kutumiwa na kukamatwa kwa wingi katika nchi za Oceania. Kiwango cha matumizi ya dawa za kulevya katika ukanda huu ni kati ya asilimia 9.1 na 14.6 ambacho ni kati ya viwango vya juu vya matumizi duniani. Australia inashika nafasi ya kwanza kwa kuwa soko la bangi katika eneo hili.

Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2011, ukamataji wa bangi nchini Australia ulifika asilimia 72 ya matukio yote ya ukamataji wa dawa za kulevya. Kwa mfano kiasi cha kilo 50,073 za bangi zilikamatwa kiasi ambacho ni kikubwa katika historia ya kipindi cha miaka 10 iliyopita. Ukamataji wa dawa ya kulevya aina ya cocaine

katika Oceania unachukua asilimia 0.3 ya jumla ya ukamataji wote duniani. Ongezeko lililojitokeza mwaka 2011 linaashiria eneo hilo kuwa soko la dawa hizo na njia ya kupitishia dawa hizo. Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2011 kiasi cha cocaine kilichokamatwa nchini Australia kiliongezeka mara mbili zaidi ya miaka iliyopita. Nchini New Zealand kilo 16.2 za cocaine zilikamatwa katika kipindi cha miezi 7 ya mwaka 2012, ambalo ni ongezeko kubwa kutoka gram 615 zilizokamatwa mwaka 2011.

Saikotropiki.

Ukamataji wa dawa za kulevy aina ya *crystal* metamfetamini wa kiasi cha kilo 306 na kilo 252 za heroin, ulifanyika Sydney mwezi Julai 2012. Kiasi hiki kikubwa cha ukamataji hakijawahi kutokea katika eneo hilo la Oceania. Kiasi hiki cha ukamataji kinaonesha ni jinsi gani matumizi ya dawa za kulevy yanaendelea kuongezeka katika eneo hili. Dawa za amfetamini zinaendelea kuingizwa nchini Australia.

Kemikali Bashirifu

Kutokana na kuboreshwa kwa sheria ya kudhibiti kemikali bashirifu hasa *ephedrine* na *pseudophedrine* nchini Australia, wahalifu wa dawa za kulevy wamegundua njia nyingine za kutengeneza dawa za kulevy aina ya amfetamini. Mwaka 2010 hadi 2011, nchi ya Australia iligundua maabara haramu 702 za kutengeneza dawa za kulevy ambayo ni idadi kubwa zaidi kuwahi kugunduliwa. New Zealand iliweza kuharibu maabara haramu 130 za kutengeneza metamfetamini mwaka 2010 ambazo ni pungufu ya zile 135 zilizoharibiwa mwaka 2009.

Dawa mpya za kulevy zinazozidi kugunduliwa

Nchini Australia mamlaka za udhibiti zinazidi kukabiliana na changamoto ya ugunduzi wa aina mpya za ATS ambalo ni tatizo linalozidi kuongezeka. Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2011 dawa mpya aina ya *ketamine* na nyingine zipatazo 22 zilizogunduliwa.

2.5.2 Matumizi na Tiba

Bangi bado inaendelea kutumiwa kwa wingi katika nchi za Oceania. Mwaka 2012 matumizi ya bangi yalipanda na kufikia asilimia 14.8 ambapo watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 walitumia bangi katika nchi za Oceania mwaka 2009. Aidha, dawa aina ya cocaine, heroin, ATS pamoja na viyeyushi ziliendelea kutumiwa.

SURA YA TATU:

3 UDHIBITI WA TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

Mwaka 2012 zilifanyika jitihada za kudhibiti biashara haramu na matumizi ya dawa za kulevya hapa nchini. Jitihada hizi zimeanishwa hapa chini kama ifuatavyo:-

3.1 Udhibiti wa Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya

Katika kudhibiti biashara haramu ya dawa za kulevya kwa mwaka 2012 kazi mbalimbali za kudhibiti biashara hiyo zilifanyika zikiwemo udhibiti wa kilimo cha mimea ya bangi na mirungi, ukamataji wa dawa za kulevya , uendeshaji wa kesi pamoja na uteketezaji wa dawa za kulevya. Shughuli nyingine ni kuimarisha udhibiti wa dawa za tiba zenye madhara ya kulevya, udhibiti wa kemikali bashirifu, udhibiti wa fedha haramu, marekebisho ya sheria na kuendelea na mchakato wa kuunda chombo madhubuti cha kupambana na dawa za kulevya.

3.1.1 Udhibiti wa Kilimo cha Mimea ya Bangi na Mirungi

Kilimo cha bangi kimeendelea kuwa tatizo kubwa hapa nchini kutokana na dawa hiyo kustawi karibu kila sehemu ya nchi yetu. Serikali imefanya jitihada ya kuteketeza mashamba ya bangi ambapo jumla ya ekari 214 ziliteketezwa na kilo 48,658 za bangi kavu zilikamatwa katika kipindi cha mwaka 2012. Halikadhalika, kiasi cha kilo 6,216 za mirungi zilikamatwa.

3.1.2 Ukamataji wa Dawa za Kulevya

Jitihada za kukamata dawa za kulevya ziliendelezwa na vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama na kuleta mafanikio kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.9. Jeshi la Polisi lilifanya misako na operesheni katika maeneo mbalimbali nchini na kufanikiwa kukamata kiasi kikubwa cha dawa za kulevya pamoja na kuwatia mbaroni watuhumiwa wa dawa hizo. Halikadhalika, Kikosi Kazi cha Kupambana na Dawa za Kulevya kilifanya uchunguzi na kuendesha operesheni dhidi ya kilimo na biashara za dawa kulevya na kuleta mafanikio makubwa. Mwezi Februari mwaka 2012 kiasi cha kilo 211 za heroin zilikamatwa kwa wakati mmoja mkoani Lindi ambapo watuhumiwa wanne walitiwa mbaroni. Aidha, ushirikiano na mataifa mengine uliimashwa ambapo jumla ya watanzania 42 walikamatwa kwa makosa ya kusafirisha dawa haramu za kulevya katika nchi mbalimbali duniani zikiwemo Japan, Kenya na Argentina.

Jedwali Na.6: Kiasi cha dawa za kulevyta zilizokamatwa, idadi ya kesi na idadi ya watuhumiwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2012.

AINA YA DAWA	UZITO (Kilo)	IDADI YA KESI	WATUHUMIWA
Heroin	260	15	400
Cocaine	151	11	138
JUMLA	411	26	538

Vilevile, raia wa kigeni wapatato 15 walikamatwa wakituhumiwa kusafirisha dawa za kulevyta. Ukomataji huu ni matokeo ya ushirikiano mzuri uliofanywa na vyombo vya dola vya hapa nchini na vile vya kimataifa vikiwemo Shirika la Polisi la Kimataifa (Interpol).

3.1.3 Uendeshaji wa Kesi na Uteketezaji wa Dawa Za Kulevyta

Kesi mbalimbali zilizohusu dawa za kulevyta ziliendeshwa na kutolewa uamuzi. Mwaka 2012, Mahakama Kuu ilitoa hukumu ya kesi ya kusafirisha kilo 92.2 za heroin ambapo washitakiwa watano walihukumiwa kifungo cha miaka 25 jela na kulipa faini ya shilingi bilioni moja, milioni mia nne thelathini na nane, laki tatu na sitini na nne elfu (Tshs. 1,438,364,000/=) kila mmoja baada ya kupatikana na hatia ya kusafirisha kiasi hicho cha dawa mkoani Tanga. Aidha, mahakama iliamuru magari mawili yaliyotumiwa kusafirisha dawa hizo yataifishwe. Sambamba na ukamataji wa dawa za kulevyta, jitihada pia zilielekezwa kuziharibu dawa za kulevyta. Kiasi cha kilo 96.88 za dawa za kulevyta zilitekezwa baada ya kutolewa hukumu za kesi husika katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Mtwara na Lindi.

3.1.4 Udhibiti wa Dawa za Tiba zenye Madhara ya Kulevyta

Katika kudhibiti dawa za tiba zenye madhara ya kulevyta serikali kupitia ofisi ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ilitoa vibali vya kuingiza na kununua dawa za tiba zenye madhara ya kulevyta kulingana na mahitaji ya nchi kwa makampuni na hospitali mbalimbali. Mwaka 2012 TFDA ilitoa jumla ya vibali 51 kwa makampuni 22 kuingiza dawa hizi hapa nchini. Vilevile, ilitoa jumla ya vibali 175 kwa hospitali mbalimbali hapa nchini kupitia Bohari ya Taifa ya Madawa (MSD). Dawa zilizoingizwa ni pamoja na *Phenorbebatone*, *Methadone*, *ephedrine* na *Pseudoephedrine* kama inavyoonyesha katika Jedwali Na.7.

Jedwali Na. 7: Dawa za tiba zenye madhara ya kulevy ya zilizoingizwa nchini mwaka 2012.

AINA YA DAWA	JINA LA KIAMBATA	KIASI KILICHOINGIZWA	NCHI ZINAKOTOKA
Saikotropiki	1. <i>Alprazolam</i>	0.069kg	India
	2. <i>Bromazepam</i>	0.49162kg	Ugiriki
	3. <i>Diazepam</i>	14.21kg	India na Kenya
	4. <i>Lorazepam</i>	0.18kg	Cyprus
	5. <i>Midazolam</i>	0.175kg	Uswisi
	6. <i>Phenorbarbitone</i>	24.45kg	Kenya na Ubelgiji
Nakotiki	1. <i>Codeine</i>	25.07104kg	Denmark
	2. <i>Morphine</i>	2.250kg	Uingereza
	3. <i>Etorphine</i>	3.6064kg	Afrika Kusini
	4. <i>Methadone</i>	9.792kg	Canada
	5. <i>Pethidine</i>	5.51145kg	Uingereza na Afrika Kusini
Kemikali Bashirifu	1. <i>Ephedrine</i>	9.104kg	Kenya
	2. <i>Pseudoephedrine</i>	1048.917kg	India, Denmark na Kenya

Pamoja na Serikali kuruhusu uingizwaji wa dawa za tiba zenye madhara ya kulevy kwa kuzingatia mahitaji ya nchi dawa hizo zimeendelea kuibwa pindi zinapokuwa chini ya uangalizi wa makampuni hayo. Kwa mfano; mwaka 2011 jumla ya kilo 25 za dawa za tiba zenye madhara ya kulevy aina ya *Pseudoephedrine hydrochloride*, kilo 5 *dizipine hydrochloride*, kilo 23.68 za *dextropropoxyphaane*, kilo 42 za *ephedrine* na kilo 14.80 za *phenorbarbitone* ziliibwa katika makampuni ya Zenufa na Tanzania Pharmaceutical LTD yaliyopo kutoka mikoa ya Dar es Salaam na Arusha. Wizi huu unaashiria uwezekano wa kuwepo kwa maabara haramu za utengenezaji wa dawa za kulevy aina ya ATS hapa nchini.

3.1.5 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu

Kemikali bashirifu zinajumuisha aina zote za kemikali ambazo hutumika kutengeneza dawa za kulevy. Mfano wa kemikali hizo ni Potassium Permanganate inayotumika kutengeneza dawa ya kulevy aina ya cocaine na acetic anhydride ambayo inaweza kutumika kutengeneza dawa ya kulevy aina ya heroin. Pamoja na kuwa kemikali hizi zinatumika kutengeneza dawa za kulevy zina umuhimu mkubwa sana katika shughuli za kiuchumi. Hivyo basi, katika kipindi cha mwaka 2012 Serikali kupitia

Ofisi ya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali ilisimamia matumizi sahihi ya dawa hii kwa kuzingatia ibara ya 12 ya mkataba wa kimataifa wa udhibiti wa dawa za kulevyta wa mwaka 1988, ambapo kemikali bashirifu zilizoagizwa na kutumika ni zile zilizowekwa chini ya uangalizi maalum ikiwa kama njia ya kuzuia zisichepushwe kwa matumizi haramu.

Jumla ya sampuli 5,228 za kemikali zilizodhaniwa kuwa dawa za kulevyta zenye uzito wa kilo 389.51 zilipimwa katika Ofisi ya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali mwaka 2012. Matokeo ya sampuli hizo yalikuwa ni kama ifuatavyo:- Sampuli 3,706 zilitoa majibu chanya kwa dawa ya kulevyta aina ya heroin, sampuli 369 dawa aina ya cocaine, sampuli 766 mchanganyiko wa dawa aina ya heroin na cocaine, sampuli 838 bangi, sampuli 79 mirungi, sampuli 3 Diazepam, sampuli 1 Cafine na sampuli 2 Nicotine. Kati ya sampuli hizo sampuli 91 zilionekana siyo dawa za kulevyta.

Jedwali Na.8: Idadi, uzito na aina ya sampuli ya dawa za kulevyta zilizopimwa na Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2012.

AINA YA DAWA	IDADI YA SAMPULI	UZITO (Kilo)	UZITO (Gramu)
Heroin	3,706	52.58	52579.95
Bhangi	838	96.87	96872.7
Cocaine	369	19.42	19419.06
Morphine	3	-	-
Diazepam	3	-	-

Matokeo ya vipimo hivi yalichukuliwa kutoka katika Ofisi ya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali na kupelekwa mahakamani ambapo hutumika kama kielelezo cha ushahidi dhidi ya kesi inayowakabili watuhumiwa.

3.2 Udhibiti wa Matumizi ya Dawa za Kulevyta

Mwaka 2012 Serikali iliendelea kufanya jitihada za kupunguza tatizo la matumizi ya dawa za kulevyta ikiwa ni pamoja na kutoa elimu juu ya athari za matumizi ya dawa za kulevyta, kutoa tiba na ushauri nasaha kwa watumiaji wa dawa za kulevyta.

3.2.1 Elimu kwa Umma

Katika Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2012, Tume ilishirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kutoa elimu juu ya athari za dawa za kulevyta kuititia ujumbe wa **“Jali afya yako usitumie dawa za kulevyta”**. Njia zilizotumika kutoa elimu kwenye mbio hizo ni pamoja na machapisho, makala zenye ujumbe

mbalimbali unaohusu dawa za kulevy. Aidha, elimu ilitolewa kupitia vyombo vya habari ambavyo ni magazeti, redio na televishen. Vilevile, elimu ilitolewa kwenye matukio maalum ya kitaifa yakiwemo Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevy Duniani ambayo huadhimishwa tarehe 26 Juni kila mwaka, Sabasaba, Nanenane, Kilele cha Mbio za Mwenge, Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani na Siku ya UKIMWI Duniani. Aidha, Tume imeendelea kutoa machapisho mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa kwa wananchi hasa kwenye maadhimsho na matukio ya kitaifa. Tume imewezesha urahisi wa upatikanaji wa taarifa za dawa za kelevy kwenye mtandao ambapo unapatikana kwenye tovuti ya Serikali <http://www.pmo.go.tz/documents/reports>.

Halikadhalika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ilitumia Baraza la Watoto la Taifa kuelimisha madhara ya dawa za kulevy na kuwajengea stadi za maisha ili kuwakinga na matumizi ya dawa hizi. Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI pia iliwaelimisha wakulima wa bangi wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma juu ya athari za kilimo cha bangi na umuhimu wa kuwafichua wakulima wa zao hilo haramu. Wizara ya mambo ya Ndani ya Nchi kupitia jeshi la magereza ilitoa elimu kwa wafungwa na mahabusu kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevy kwa kutumia wataalam wao wa afya.

Tume ya Kuratibu na Uthibiti wa Dawa za Kulevy Zanzibar ilitoa elimu kwa wanafunzi 7,545 kwenye skuli 65 za Unguja na Pemba. Aidha, Tume ilianda programu na ziara za uhamashaji kupitia vyombo vya habari na skuli mbalimbali kwalengo la kuihamashishi jamii kuunga mkono juhudzi za Serikali juu ya mapambano dhidi ya dawa za kulevy ambapo jumla ya vipindi 45 vilitolewa hewani, 35 redioni na 10 kwenye televisheni.

Asasi ya Manzese Youth Group ilitoa elimu kwa vijana 784 juu ya Athari za utumiaji wa Dawa za kulevy na VVU/UKIMWI katika vijiwe vya watumiaji na wanaofanya biashara ya kuuza Mwili, katika wilaya ya Kinondoni maeneo ya Hananasifu, Kinondoni Shamba, Tandale kwa Ally Maua na uwanja wa fisi.

Asasi ya Green Hope Youth Organization ya Mwanza imeweza kutoa elimu katika mkoa huo kwa jumla ya wananchi 4,509 wakiwemo vijana wanaotumia na wasiotumia dawa za Kulevy kuhusu madhara ya dawa za kulevy na VVU/UKIMWI.

Taasisi ya Tanzania IOGT ilitoa elimu ya dawa za kulevy katika shule nne za sekondari katika manipaa ya Kinondoni na shule tatu za msingi katika manipaa ya Temeke kupitia mkusanyiko wa pamoja kwa siku maalum kwa njia ya michezo na utamaduni. Taasisi ya T- IOGT pia ilianda makambi maalum kwa wanafunzi wakati wa likizo ambapo walipewa elimu ya dawa za kulevy. Taasisi hii ilianzisha klubu za kudumu kwa ajili ya majadiliano kuhusu dawa za kulevy kwenye shule

zilizopewa elimu. Aidha, elimu juu ya athari za dawa za kulevyta ilitolewa kwenye vyama veya michezo ya riadha na ngumi katika jiji la Dar es Salaam.

Asasi ya Guluka Kwalala ya Manispaa ya Ilala ilitoa mafunzo juu ya dawa za kulevyta kwa watoto wa mitaani 105 na vijana 117 walipata elimu ya dawa za kulevyta. Halikadhalika, elimu ya dawa za kulevyta ilitolewa kwa kata tatu za Wilaya ya Mkuranga na kata nne za wilaya ya Kisarawe ambapo jumla ya watu 380 walifaidika na elimu hiyo.

Asasi ya Youth and Community Rehabilitation (YCR) ilitoa elimu kwenye semina na warsha katika asasi ya Jitambue iliyopo Gongo la Mboto, shule ya Ufundji Mikocheni, kijiji cha Gezaulole, Kinondoni Baptist Church na Kibasila Sekondari ambapo jumla ya watu 392 walifaidika na elimu hiyo. Asasi ya YCR pia ilitembelea vijiwe 25 katika manispaa ya Kinondoni na kutoa elimu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevyta.

Asasi ya Changamoto ni Matumaini iliweza kuwahifadhi vijana 102 kwenye nyumba ya upataji nafuu (Sober House) na kushiriki uelimishaji uliofanyika kwenye maadhisho ya Siku ya Kupiga Vita dawa za Kulevyta Duniani mwaka 2012. Kikundi cha Jikinge Arts kilitoa elimu ya dawa za kulevyta kwenye jamii kupitia sanaa ambapo wazazi walihamasika kuongea na watoto wao kuhusu madhara ya dawa za kulevyta. Kwaya ya Nazareth ya Dar es Salaam walitoa elimu kwa njia ya sanaa na kugawa vipeperushi katika Manispaa zote za jiji la Dar es Salaam pamoja na mikoa ya Tanga na Morogoro.

Asasi ya Sober Tanzania iliweza kuwapatia elimu ya dawa za kulevyta vijana takribani 1800 kupitia mafunzo, ushauri, midahalo, “outreach service” na maadhisho ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevyta Duniani.

Katika Jiji la Tanga elimu ya dawa za kulevyta ilitolewa kwenye maadhisho ya miaka 51 ya Uhuru, Mbio za Mwenge wa Uhuru na kwenye televisheni ya Tanga, redio Mwambao, Breeze FM na redio huruma za Tanga. Aidha, elimu ilitolewa kwa wazazi, watendaji wa vyombo veya usalama, nyumba za ibada, na vikao veya kata juu ya madhara ya dawa za kulevyta na kufahamisha jamii kuwa watumiaji wa dawa za kulevyta ni wagonjwa wanaohitaji kusaidiwa ikiwemo kupelekwa kwenye vituo veya ushauri.

3.2.2 Matibabu ya Utegemezi na Urekebishaji Tabia

Katika kipindi cha Januari hadi Disemba 2012 watumiaji wa dawa za kulevyta walifika katika vituo veya afya na asasi mbalimbali ili kupata tiba juu uraibu. Kwa mfano; Mkoani wa Tabora watumiaji wapatao 130 wakiwemo wanawake 21 walipata tiba katika vituo veya tiba veya wilaya za Igunga, Urambo, Sikonge, Uyui, Nzega na Manispaa ya Tabora.

3.2.2.1 Huduma kwenye Vituo vya Afya vya Manispaa na Majiji

Huduma kwa waathirika katika vituo mbalimbali vya afya vya ngazi tofauti ziliendelea kutolewa ambapo jumla ya watumiaji wapatao 914 walifikiwa jijini Mwanza. Kati yao 10 walikuwa na umri chini ya miaka kumi, 577 walikuwa na umri kati ya miaka 16 hadi 45 na 327 walikuwa na umri zaidi ya miaka 45.

Tathmini ilifanyika mkoani Iringa na Njombe ili kujua dawa za kulevyta zinazotumiwa zaidi mkoani hapo. Aidha, Katika tathmini hiyo ilionekana kuwa wanaume ndio watumiaji zaidi kuliko wanawake. Utafiti wa kina kwa mikoa hiyo unahitajika ili kujua ukubwa wa tatizo. Jumla ya waathirika 41 walipatiwa huduma mbalimbali katika vituo vya afya vya mikoa hiyo. Mkoa wa Lindi uliwhahudumia waathirika wa bangi na pombe wapatao 30. Jiji la Tanga liliweza kuwatambua waathirika wapatao 836 wanawake wakiwa 39 ambapo waraibu wapatao 25 walipatiwa matibabu katika kituo cha Pongwe ili waweze kuendelea na mikutano ya upataji nafuu.

Mwaka 2012 watumiaji wa dawa za kulevyta wanaokadiriwa kufikia 1461 walihudumiwa katika vituo vya afya vya manispaa na majiji nchini. Mchanganuo wa watumiaji waliopatiwa huduma ya tiba katika majiji na manispaa umeainishwa katika jedwali lifuatalo:-

Jedwali Na.9: Watumiaji wa Dawa za Kulevyta waliofikishwa katika vituo vya tiba ya afya ya akili na dawa za kulevyta kwa mwaka 2012

MAHALI	ME	KE	JUMLA	UMRI		
				0-15	16- 45	45>
Jiji la Tanga	836	39	836	64	671	101
Jiji la Mwanza	300	122	422	10	577	327
Mkoa wa Iringa	41	2	43	0	37	4
Mkoa wa Tabora	108	21	130	0	100	10
Mkoa wa Lindi	30	0	30	0	29	1
Jumla	1315	184	1461	74	1414	443

Huduma za tiba zilizotolewa na mashirika na asasi za kiraia

Asasi ya Guluka Kwalala iliwapa huduma ya ushauri nasaha watumiaji wapatao 70 wakiwemo wanawake 24. Jumla ya waathirika 930 wa dawa za kulevyta walipatiwa huduma mbalimbali na asasi ya YOVARIBE ikiwa ni pamoja na ushauri nasaha, na upimaji wa VVU.

Katika kutekeleza jukumu la kurekebisha tabia kwa waathirika wa dawa za kulevyta, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitenga

Tshs.10,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ili kuzikimu nyumba za kusaidia upataji nafuu kwa wateja za Zanzibar Youth Forum, Nyarugusu, Bububu, Bombay, Twawabina, Detroit, Chukwani kwa Unguja na Limbani na Mkoroshoni kwa Pemba.

Asasi na taasisi mbalimbali zilishiriki katika kutoa tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevyta kwa njia mbalimbali. Asasi ya YOVARIBE- (Youth Volunteers Against Risk Behaviours) kupitia mradi wa TAPP- (Tanzania AIDS Prevention Programme) iliweza kuwahudumia watumiaji wa dawa za kulevyta wapatao 4,414 kwa kuwapatia huduma za ushauri, kupima Virusi vya UKIMWI, kupewa kondomu, kusimamia mikutano ya watumiaji wa pombe na dawa za kulevyta (Alcoholic Anonymous na Narcotic Anonymous) wanaosaidiana kuacha, na kupewa rufaa ya huduma nyingine wanazohitaji. Watumiaji hawa walifikiwa kupitia huduma za mikoba (outreach services) kwenye kata saba za wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam. Pia, Asasi ya Kikale Youth Care Organization ya Rufiji, mkoani Pwani ilitoa tiba ya ushauri kwa watumiaji wa dawa za kulevyta wapatao 15 Msasani jijini Dar es Salaam.

Kituo cha afya cha Pongwe kilichopo jijini Tanga, kilitoa huduma ya matibabu ya kuondoa arosto mwilini ambapo watumiaji wa dawa za kulevyta wapatao 25 walipewa huduma hiyo. Aidha, katika kituo cha Afya cha Ngamiani watumiaji wa dawa za kulevyta waliweza kupatiwa ushauri na dawa za kutuliza maumivu. Kituo hiki pia kiliratibu mikutano ya NA mara mbili kwa wiki kwa watumiaji wa dawa za kulevyta. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga aliwatembelea watumiaji wa dawa za kulevyta kituo cha afya Ngamiani na kuwahamasisha kufanya huduma za mikoba kwa vijana wengine ili waachane na matumizi ya dawa hizo. Sober house kwa jina la Tanga Sober house Recovering School ilifunguliwa eneo la Duga, Manispaa ya Tanga kwa ajili ya upataji nafuu kwa wanaume wanaotumia dawa za kulevyta.

Asasi ya Youth and Community Rehabilitation ilitoa huduma ya ushauri kwa watumiaji wa dawa za kulevyta kwenye vijiwe visivyopungua 12 jijini Dar es Salaam na baadhi yao walipewa rufaa kwenda Sober house za Zanzibar. Asasi ya TAYOHAG ilisimamia uendeshaji wa mikutano ya AA na NA kwa vijana 72. Aidha, vijana 36 waliokuwa wanatumia dawa za kulevyta walipatiwa ushauri ulioratibiwa na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevyta. Asasi ya Kimara peers iliawezesha wajidunga sindano 187 kuingia kwenye tiba ya methadone.

3.2.2.2 Huduma ya Tiba ya Methadone

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani kupitia Kituo cha Kudhibiti Magonjwa ya Binadamu CDC (Centers for Disease Control and Preventions) imeendelea kuiwezesha Tume kusimamia uanzishwaji wa huduma ya MAT (Medically Assisted Treatment) katika Hospitali ya Mwananyamala ambapo Waziri wa Afya Mhe. Dr. Hussein Mwinyi (Mb) pamoja na Mhe. Balozi Alfonso

Lenhardt, Balozi wa Marekani Nchini walifungua kituo hicho Septemba 7, 2012. Kufikia Disemba 2012 jumla ya watumiaji wapatao 41 walisajiliwa kupata tiba hiyo.

3.3 Masuala Mtambuka

Tume ya Kuratibu Udhibiti Dawa za Kulevyta iliendelea utekelezaji wa masuala mtambuka kwa kufanya kazi zifuatazo:-

3.3.1 Uboreshaji wa Mfumo wa Udhibiti wa Dawa za Kulevyta Nchini

Kwa mwaka 2012 mchakato wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa dawa za kulevyta nchini uliendelea kwa kukamilisha rasimu ya Sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevyta na kuandaa rasimu ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevyta.

3.3.2 Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Biashara Haramu ya Dawa za Kulevyta [Sura 95].

Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevyta ilifanyiwa marekebisho mwezi Aprili 2012 ili kuimarisha udhibiti wa dawa za kulevyta. Katika marekebisho hayo makosa yanayohusiana na usafirishaji wa dawa za kulevyta za viwandani pamoja na kumiliki eneo linalozalisha dawa za kulevyta yalipewa adhabu ya kifungo cha maisha bila faini. Aidha, makosa ya dawa za kulevyta yalipewa adhabu inayoendana na ukubwa wa makosa husika.

3.3.3 Ushirikiano na Asasi za Kiraia

Mwaka 2012 Tume ilishirikiana na asasi za kiraia zinazojihusisha na udhibiti wa dawa za kulevyta kutoa elimu juu ya athari za dawa za kulevyta. Aidha, asasi zipatazo 16 ziliwezeshwa jumla ya Tshs. 8,940,000 zikiwemo TAYOHAG, Pilimissanah Foundation, Nazareth Kwya, Manzese Youth Group, Peer to Peer Support Group, CODATZ, Youth and Community Rehabilitation, Blue Cross Tanzania, Kimara Peer Educators, YOVARIBE, CHRP,PEDDEREF, Hatima ya Vijana Katika Jamii-Dodoma, DCMC, Sober Tanzania- Dodoma pamoja na Viongozi wa Dini. Halikadhalika, asasi zipatazo 9 ziliwezeshwa vitendea kazi zikiwemo Youth and Community Rehabilitation, Sober Tanzania, Tanga Drug Free, TAYOHAG, Ntarama Foundation,Tawabina Foundation, PEDDEREF, YCRC na Pilimissanah Foundation.

SURA YA NNE

4 UDHIBITI WA MAAMBUKIZI YA VVU MIONGONI MWA WATUMIAJI

4.1 Mazingira Wezeshi ya Utoaji Huduma

Huduma mbalimbali kwa watumiaji wa dawa za kulevyta zilitolewa ili kuwakinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI zikiwemo; huduma za tiba kwa kutumia dawa aina ya methadone, tiba ya kifua kikuu, utoaji wa dawa ya kupunguza makali ya UKIMWI, huduma ya mabomba kwa wajidunga, huduma ya magonjwa ya ngono na utoaji wa elimu kwa walengwa. Asasi na taasisi mbalimbali zilishiriki kutoa huduma hizo kama vile asasi za YOVARIBE, CHRP, Blue Cross, MDM, TAYOHAG na Kimara Peer Educators. Kazi hii ililenga kutekeleza Mkakati wa Pili wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (2008-2012) katika kuweka mazingira ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamani ya mwitikio wa kitaifa dhidi ya UKIMWI kwa misingi ya haki za binadamu na usawa wa jinsia, uwazi pamoja na uwajibikaji katika ngazi zote, ushiriki mkubwa wa jamii na uwezeshaji wa watu wanaoishi na VVU.

4.2 Uboreshaji wa Mbinu za Kuwfikia Watumiaji

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iliweka mkakati wa kuwatambua watoto wa mitaani ili kuwapatia haki mbalimbali ikiwa ni pamoja na Haki ya Kuishi, Haki ya Kulindwa, Haki ya Kuendelezwa, Haki ya Kushiriki na Haki ya Kutobaguliwa ili kuwakinga na majanga mbalimbali ikiwa ni pamoja na dawa za kulevyta na maambukizi ya VVU. Aidha, ili kuwakinga watoto dhidi ya madhara ya dawa za kulevyta mambo mbalimbali yametekelawa ikiwa ni pamoja na Rasimu ya Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto pamoja na kuanzishwa kwa Baraza la Watoto kwa lengo la watoto kuelimishana mambo mbalimbali yakiwemo madhara ya dawa za kulevyta na maambukizi ya VVU.

Vilevile, mkoa wa Rukwa uliwezesha polisi jamii pamoja na asasi mbalimbali kutoa elimu juu ya madhara ya dawa kulevyta katika halmashauri ya mkoa huo. Aidha, kauli mbiu ya mbio za mwenge kwa mwaka 2012 iliyobeba suala la dawa za kulevyta na maambukizi ya VVU iliwezesha na kuboresha mbinu mpya ya kuwfikia waathirika wa dawa za kulevyta kwa mkoa huo.

4.3 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (2008-2012) ulifanyika kwa kushirikisha wadau wote zikiwemo taasisi zilizo chini ya wizara ya afya, asasi za kiraia na wadau wengine chini ya uangalizi wa asasi ya PANGAEA ya Marekani.

Kufuatilia utoaji wa huduma ya matibabu kwa wajidunga wa heroin katika Hospitali ya Mwananyamala kwa kupata idadi ya watumiaji waliosajiliwa, wanaoendelea na tiba na walioacha tiba hiyo kwa muda kwa kutumia mfumo wa ukusanyaji taarifa uliowekwa hospitalini hapo kwa uangalizi wa wataalam kutoka PANGAEA.

SURA YA TANO:

5 MAFANIKIO, MATATIZO, CHANGAMOTO, MIKAKATI YA BAADAYE NA MAPENDEKEZO

Jitihada za udhibiti wa matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevyta kwa mwaka 2012 zilikuwa na mafanikio licha ya kuwepo kwa changamoto na matatizo mengi. Kutokana na ugumu huu, mikakati na mapendekezo ya kuimarisha jitihada za kudhibiti tatizo la dawa za kulevyta nchini yametolewa.

5.1 Mafanikio

- i. Kukamatwa kwa kiasi kikubwa cha dawa za kulevyta kwa mara moja ambacho hakikuwahi kukamatwa nchini cha kilo 211 za herion mkoani Lindi.
- ii. Kuanzishwa kwa kituo cha kutoa tiba ya methadone kwa watumiaji wa heroin katika Hospitali ya Mwananyamala;
- iii. Kuwezesha ukarabati jengo litakalotumika kutoa tiba ya methadone kwa watumiaji wa heroin katika hospitali ya Temeke;
- iv. Kuwezesha utoaji wa mafunzo kwa watoa huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevyta;
- v. Kuandaa miongozo ya utoaji huduma za matibabu kwa watumiaji dawa za kulevyta;
- vi. Kutoa elimu ya kisheria kwa watumiaji wa dawa za kulevyta;
- vii. Kuanzisha uundai wa mfumo wa ufuutiliaji na tathmini ya jitihada za kupunguza matumizi ya dawa za kulevyta;
- viii. Kufuatilia mwenendo wa kesi za dawa za kulevyta ikiwemo iliyohusisha kiasi kikubwa cha dawa hizo mkoani Tanga;
- ix. Uelimishaji umma juu ya madhara ya matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevyta kuititia vyombo vya habari, mikutano ya vijana na matukio maalum ya kitaifa yakiwemo maonesho ya Wakulima -Nane Nane, Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani, Wiki ya Vijana na Kilele cha mbio za mwenge na siku ya UKIMWI Duniani;
- x. Kukamilisha rasimu ya Sera ya Taifa ya Udhibiti wa Dawa za Kulevyta Nchini.
- xi. Kushirikiana na asasi za kiraia katika udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevyta kwa vijana na jamii kwa ujumla;

- xii. Kushirikiana na asasi za kiraia katika kuanzisha huduma za upataji nafuu (Sober houses) kwa watumiaji wa dawa za kulevya.

5.2 Changamoto na Matatizo

- i. Ukosefu wa taarifa sahihi kuhusu tatizo la matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini;
- ii. Kupungua kwa rasilimali zinazoelekezwa kwenye udhibiti wa dawa za kulevya;
- iii. Kupanda kwa gharama za uendeshaji wa vipindi kwenye vyombo vyahabari;
- iv. Mahitaji makubwa ya huduma za tiba kwa watumiaji ukilinganisha na uwezo uliopo;
- v. Unyanyapaa na kubaguliwa kwa watumiaji wa dawa za kulevya;
- vi. Uhaba wa wataalam na miundo mbinu ya kuwezesha utoaji wa huduma za tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya;
- vii. Kushamiri kwa kilimo cha bangi pamoja na kilimo hicho kufanyika katika maeneo yasiyofikika kiurahisi;
- viii. Kuwepo kwa mipaka mingi yenye vipenyo visivyo rasmi na ukanda mrefu wa pwani hali inayorahisisha uingizaji wa dawa za kulevya nchini;
- ix. Wananchi kutoshiriki kikamilifu katika vita dhidi ya dawa za kulevya, kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo hofu ya kudhuriwa na wafanyabiashara wa dawa hizo pamoja na uelewa mdogo wa tatizo hili.
- x. Wafanyabiashara wa dawa za kulevya kubadili mbinu za usafirishaji wa mara kwa mara.

5.3 Mikakati ya Baadee

- i. Kuendelea na ufunguzi wa kituo kingine cha tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya katika Manispaa za Temeke;
- ii. Kuandaa mwongozo wa kuendesha nyumba za upataji nafuu;
- iii. Kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa huduma kwa watumiaji wa dawa za kulevya;
- iv. Kuongeza uwezo wa kiutendaji kwa kuwapatia mafunzo wataalam wanaotoa kwa watumiaji wa dawa za kulevya; na
- v. Kuimarisha ushirikiano na wadau katika kudhibiti dawa za kulevya ndani na njie ya nchi.

5.4 Mapendekezo

- i. Kuimarisha mahusiano ya vyombo vya dola katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya.
- ii. Tatizo la dawa za kulevya litangazwe kuwa janga la taifa ili kuleta hamasa kwa wananchi kushiriki katika mapambano.
- iii. Zifanyike tafiti za kutosha kuhusu tatizo la dawa za kulevya ili kujua ukubwa wa tatizo na kuwezesha mipango sahihi ya udhibiti.
- iv. Kuanzishwa mahakama maalum ya kesi za dawa za kulevya.
- v. Kuongeza bajeti ya kupambana na dawa za kulevya.

ISBN: 978-9987-9596-4-8

**Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevyा,
Kitalu Namba 434, Barabara ya Malik, Upanga,
S.L.P. 80327, Dar es Salaam - Tanzania
Simu: +255 22 2152532 | Tarakilishi: +255 22 2152820
Barua pepe: tumedawa@pmo.go.tz | Tovuti: www.pmo.go.tz**